epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Agosti 8, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581762
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 21

**BAYERN MUNICH KUMPIGA BEI ALPHONSO DAVIES**

UKURASA WA 3

**Ripoti** huduma kibingwa yataja magonjwa tishio

UKURASA WA 5

**Siku** 13 ICU za kuokoa maisha mtoto aliyekatwa koo na hausigeli



UKURASA WA 5

**ACT** Wazalendo yapendekeza mwarobaini migogoro ardhi



# Mapya yaibuka binti aliyedaiwa kubakwa

• **Aliyemzushia** kwamba amefariki dunia atiwa mbaroni... *Endelea ukurasa 3*

UKURASA WA 22

## ONANA AAHIDI FURAHA KWA MASHABIKI

**LOS ANGELES,** Marekani

MLINDA mlango wa Manchester United, Andre Onana, amebainisha kuwa ana...





Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuzindua rasmi Kiwanda cha Sukari Mkulazi, Mbigiri mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

## Samia asimulia alivyoumia kupanda bei sukari

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

# Uzoaji wa taka ulivyogeuka kitendawili, tishio kwa afya

UK. 4

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA SC HAPATOSHI LEO** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Samia asimulia alivyoumia kupaa bei ya sukari

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema alipata tetemeko la maumivu wakati bei ya sukari ilipouzwa Sh. 8,000 kwa kilo, kulikosababishwa na baadhi ya wafanyabiashara kuficha bidhaa hiyo.

Amesema wakati huo viwanda vya kuzalisha sukari vilishindwa kufanya uzalishaji kutokana na mvua nyingi zilizonyesha kuanzia Januari hadi Aprili mwaka huu.

Rais alisema hayo jana wakati akizindua kiwanda cha Mkulazi I mkoani hapa, kilichogharimu Sh. bilioni 340 ambacho kinamilikiwa kwa pamoja kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Jeshi la Magereza.

Akiwa katika kiwanda hicho, Rais Samia aliagiza kuanza kwa ujenzi wa kiwanda kipya cha Mkulazi II kilichopo Ngerengere Wilaya ya Morogoro ili taifa liwe na usalama wa chakula baada ya kukamilika na kuanza uzalishaji wa tani 50,000 kwa mwaka wa Kiwanda cha Mkulazi I kilichopo Mbigiri Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro.

Aidha aliauagiza uongozi wa Kiwanda cha Mkulazi I kutoogopa mkono wa mtu yeyote kutoka juu na badala yake kufanya kazi kwa kusimamia sera, sheria, taratibu na kanuni kuwa endelevu.

"Nadhani ilikuwa kati ya Januari na Aprili nilipatwa na tetemeko kidogo zilipoanyesha mvua nyingi, viwanda havikuzalisha lakini sukari kwenye baadhi ya maeneo ilikuwepo lakini watu wakabana na sukari ikapanda bei kupindukia hadi Sh. 8000 kwa kilo moja kiasi ambacho Mtanzania wa kawaida asingeweza kumudu" alisema Rais Samia.

Alisema kiwanda hicho ni cha pekee kutokana na kumilikiwa na taasisi za serikali na kwamba atahakikisha anakitafutia fedha ili kiongeze uwezo wa kuzalisha sukari kutoka tani 50,000 hadi tani 75,000 kwa mwaka.

Kukiwa na viwanda vya serikali vya aina hiyo, alisema hata ikinyesha mvua kubwa na viwanda kushindwa kuzalisha serikali itaweza kutoa sukari iliyohifadhiwa bila mgogoro kwa ajili ya kuwauzia wananchi kwa bei ya kawaida.


"Waliothirika zaidi wakati ule wa bei ya sukari kupandishwa wanaofanya biashara ndogo ambao ni kina mama lishe pamoja na watoto ambao wanatumia sukari, sisi watu wazima ukifika umri fulani unapunguza matumizi ya sukari kwakuwa inaweza kukuletea athari" alisema .

Rais Samia alisema ujenzi wa Mkulazi II utakwenda kuipa serikali uhakika wa chakula na sukari hapa nchini, hivyo serikali inakwenda kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo hata kama itashirikiana na seka binafsi.

Alisema tayari ujenzi wa awali wa kiwanda hicho umeshatumia Sh. bilioni 2.6 na kutaka wawekezaji au sekta binafsi ambao wapo tayari kushirikiana na serikali kujitokeza.

Rais alisema serikali imeamua kuipa jukumu Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua sukari kadri itakavyokuwa na uwezo wa kuifadhi ili inapotekea upungufu wananchi waweze kupata huduma.

"Nazipongeza hizi taasisi za serikali kwa kuamua kuwekeza kwenye mradi huu wa ujenzi wa kiwanda cha sukari, kwani mtawasaidia wananchi pale patakapokuwa na upungufu wa sukari," alisema.



Aidha, Rais Samia alisisitiza umuhimu wa uendelevu wa mradi huo akisema uzoefu unaonyesha kitu kinapokuwa cha serikali umakini wake unakuwa mdogo, akitolea mfano kufa kwa viwanda vingi vya serikali katika miaka ya nyuma.

"Yako mambo tu kitu kikiwa cha Serikali basi umakini wake unakuwa mdogo, sasa hapa nimepokewa na kijana mahili sana nadhani ni Mtendaji Mkuu wa Kiwanda cha Mkulazi, nataka kumwambia kuwa asimamie kwelikweli mradi uwe endelevu, kama kutakuwa na mkono wowote unatoka huko juu kwetu kuingiza simamia sera, kanuni na taratibu na usimame hapo" alisema Rais Samia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Dk. Hildelitha Msita, alimwomba Rais Samia kukiongezea nguvu ya kifedha kiwanda hicho ili uzalishaji wake ufike tani 75,000 kwa mwaka.

Alisema kiwanda hicho kimejengwa kwa teknolojia ya hali ya juu na kina uwezo wa kuchakata miwa tani 500,000 sawa na uzalishaji wa tani 50,000 za sukari kwa mwaka.

Dk. Msita alisema uzalishaji wa sukari kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ulianza Julai Mosi mwaka huu kwa tani 200 hadi 250 kwa siku .

Alisema kampuni ina mipango ya kupanua wigo wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na miwa na kwa kuanzia wanaaza na kuzalisha ethanol ambayo inaweza kutumika katika matumizi mbalimbali ikiwemo malighafi ya kutengeneza dawa.

Hatua hiyo, alisema itaiwezesha kampuni kuongeza mapato na kushusha bei ya sukari na hao ni mipango na matarajio ya kampuni katika kuleta maendeleo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Ridhiwan Kikwete, alisema ujenzi wa kiwanda hicho utatatua tatizo la ajira kwa vijana.

Alisema kiwanda hicho kimetoa ajira 2,176 ambazo ni rasmi na 7,000 zisizo rasmi. Alisema kiwanda hicho pia kinakwenda kuongeza makusanyo katika mapato na kutatua changamoto ya upungufu wa sukari.

Naye Waziri wa wa Kilimo, Husein Bashe, aliwaahidi wakulima wa miwa ambao walipeleka miwa katika kiwanda hicho na wanaodaiwa na Benki ya Azania kuwa suala lao linashughulikiwa.

Mwenyekiti Chama cha Wakulima wa Miwa wa Nje Mbigiri wilayani Kilosa, Salome Mbilinyi, alishukuru serikali kwa uwekezaji wa kiwanda hicho na kuomba changamoto zao kutatuliwa.

TOL Gases PLC since 1950 We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P. O. Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, E – mail: info@tol-gases.co.tz

TAARIFA

MKUTANO WA 29 WA WANAHISA WOTE

**TAARIFA INATOLEWA HAPA** kuwa Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wote wa TOL Gases PLC utafanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City Dar es Salaam na kwa njia ya mtandao wa ZOOM, siku ya tarehe 29 Agosti 2024, kuanzia saa 3.00 asubuhi kufanya shughuli zifuatazo:-

1. Kuikubali Ajenda.
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa. uliofanyika tarehe 25 Agosti, 2023.
3. Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano wa 28 wa Wanahisa.
4. Taarifa ya Mwenyekiti.
5. Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi, Ripoti ya Wakaguzi wa Mahesabu na Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2023.
6. Malipo ya Gawio.
7. Kuidhinisha Ada za Wakurugenzi.
8. Kuteua Wakaguzi wa Mahesabu kwa mwaka 2024.
9. Kuteua Wakurugenzi.
10. Kupanga sehemu na tarehe ya Mkutano Mkuu wa 30 wa Wanahisa.
11. Mengineyo (yaliyotaarifiwa rasmi angalau siku saba kabla ya mkutano).

Kujisajili ili kushiriki mkutano kwa njia ya mtandao kutafanyika kupitia namba **0685750201/0685750203**

Mwanahisa anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano huu anaruhusiwa kuteua mtu mwingine (awe Mwanahisa wa Kampuni au la) kuhudhuria na kupiga kura badala yake.

Fomu zote za uwakilishi (proxy forms) ama barua za kuteua wawakilishi zifikishwe katika ofisi ya Katibu wa Kampuni angalau saa 48 kabla ya muda uliopangwa kufanyika mkutano au kupitia email **mjuliana@tol-gases.co.tz / nlulu@tol-gases.co.tz**

**KWA AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI.**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**

Directors: H. Kitilya – Chairperson (Tanzanian), T. Kinabo - (Tanzanian), J. Massawe – (Tanzanian), L. Kitoka (Tanzanian) S. Selestine – TR - URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzania)

TANGAZO LA NOTISI - MDAIWA

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Thelathini (30) kwa mdaiwa, Ndugu **LIGWA SHIBILITI NHOGOLO,** wa Nyasaka Wilaya ya Nyamagana- Mwanza.

**LIGWA SHIBILITI NHOGOLO** ulikopa na kushindwa kulipa deni la mkopo wako, hivyo unatakiwa kulipa deni lako la mkopo unaodaiwa na Tujijenge ndani ya siku thelathini (siku30). Hii ni baada ya mkopo kushindwa kulipwa kulingana na masharti na makubaliano ya mkataba.

Notisi hii ya siku thelathini (30) itatumika kuanzia tarehe ya Tangazo hili gazetini. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa dhidi yako endapo kama utashindwa kulipa deni la mkopo ndani ya muda ulioainishwa (siku thelathini).

Ikiwa ni pamoja na kuruhusu dalali kuendelea na taratibu za kisheria za kuuza mali zako zilizotumika kudhamini mkopo uliochukuliwa.

Kwa Mawasiliano piga: +255222774742-3/0677088251/ 0718068335
Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz

HABARI KITAIFA




Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, kuhusu kukamatwa kwa Mkazi wa Tegeta, Amos Lutahembelwa kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo juu ya kifo cha binti anayedaiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mapya yaibuka binti aliyedaiwa kubakwa

**Na Romana Mallya**

MAPYA yameibuka kuhusu tukio la unyanyasaji wa kingono binti, mkazi wa Yombo Dovya, Temeke, mkoani Dar es Salaam, ambaye baada ya ukatili uliofanyika dhidi yake, ameondolewa katika nyumba aliyokuwa amepanga.

Wakati hayo yakiibuka, wadau mbalimbali wa haki za binadamu na wanasaikolojia, wameendelea kujitokeza na kulaani kitendo alichofanyiwa binti huyo na kutaka sheria zichukuliwe dhidi ya wahusika na kwa uwazi.

Bintu huyo anadaiwa kufanyiwa ukatili huo na vijana watano na video yake kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii, kwa kile walichodai kuwa walitumwa na bosi wao kwamba alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alipoulizwa jana na Nipashe walikofikia kuhusu kumfuatilia binti huyo ili kumsaidia kisheria, alisema baada ya kwenda wameambiwa nyumba aliyokuwa akiishi ameondolewa.

"Hatujampata. Timu yangu iliyokwenda kule Yombo Dovya, ilifika hadi ofisi ya serikali ya mtaa alikokuwa anakaa, wakasema binti huyo ameondolewa na hawajui yuko wapi. Alikuwa mpangaji kwenye moja ya nyumba huko.

"Alikuwa anakaa na mama yake ambaye alikuwa mgonjwa sana. Licha ya kwamba hatujampata, tunasubiri kesi itakapofikishwa mahakamani tutamsaidia msaada wa kisheria," alisema.

**WAZIDI KULAANI**

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania, Sheikh Alhad Mussa Salum, alisema tukio hilo ni la kinyama na kishenzi ambalo halijazoeleka ndani ya jamii na limebeba ukatili na udhalilishaji.

"Hata kama alitenda kosa hilo bado alilotendea ni ukatili ambao haupaswi kutendwa. Kama viongozi wa dini tunalilaani. Vijana wasitumike vibaya hapo mtu ana dhambi mara mbili ya kuzini na kumtendea mtu ukatili," alikumbusha.

Sheikh Salim aliwasihi vijana wasikubali kuiga vitendo visivyofaa na wawe na hofu ya Mungu.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili na Kilutheri (KKKT), Dk. Emmanuel Mlyuka, ambaye ni mnasihi, alisema tukio hilo ni kiashiria kikubwa kuwa mmomonyoko wa maadili umeporomoka katika jamii.

"Kukosekana kwa hofu ya Mungu ambayo ni tatizo la kiroho, huondoa utu na kutomjali binadamu mwingine na kushindwa kumchukulia kama binadamu na kumwona kama mnyama. Hicho ni kitendo cha ukatili," alisisitiza.

Pia alisema kitendo hicho kinaashiria changamoto ya afya ya akili kwa vijana kwa sababu mwenye akili timamu hawezi kufanya jambo hilo kwa kujirekodi na kutuma.

"Hili ni jambo linalopaswa kukemewa, wahusika wanapaswa kuchukuliwa hatua na umma ujue kwamba, wamechukuliwa hatua na taarifa zitolewe ili kudhibiti vitendo hivyo na kuwa fundisho kwa wengine," alisema.

Alisema hatua zichukuliwe bila kuangalia sura ya mtu ili kutunza maadili ya taifa, kwa kuwa husambaa duniani na kuleta aibu na yana maumivu ya kisaikolojia na mwili kwa mhusika pamoja na familia.

"Huyu binti anahitaji msaada wa kisaikolojia ili kulinda afya yake ya akili vinginevyo tutampoteza. Wazazi wake wanajisikiaje? Nao wameathirika wanahitaji kusaidia kupata msaada wa kisaikolojia.

"Kama sisi tumeumia kiasi hiki unadhani wazazi, wadogo zake, wameumiaje? Wanahitaji msaada pia wa kiroho ili kuwalinda wasipate matatizo mengine," alishauri.

Agosti 4, mwaka huu, katika mitandao ya kijamii kulisambaa video ikionesha namna vijana watano wakimfanyia ukatili huo binti huyo huku wakimrekodi.

Katika video hiyo vijana hao walisikika wakimtuhumu kutembea na mume wa mtu na binti huyo akisikika kuomba msamaha mtu aliyetambulishwa kama afande.

**ALIYEMZUSHIA MBARONI**

Jeshi la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linamshikilia na kumhoji Amos Lwiza (54), mkazi wa Tegeta, Dar es Salaam kwa tuhuma za kuzusha na kusambaza taarifa za uongo kwenye mitandao ya kijamii kwamba binti aliyebakwa na kulawitiwa amekutwa amefariki dunia.

Video tatu za tukio la kubakwa na kulawitiwa linalodaiwa kufanywa na askari watano wa vyombo vya ulinzi na usalama ambao walidai kutumwa na bosi wao, zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii Agosti 4, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalimu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema taarifa zilizotolewa na mtuhumiwa Lwiza baada ya kuchunguzwa, zimebainika kuwa za uongo na zilikuwa na lengo la kuzusha taharuki na kuingilia uchunguzi wa tukio hilo.

"Shauri kuhusu binti huyo bado linachunguzwa na liko katika hatua za mwisho na taarifa yake itatolewa na msemaji wa Jeshi la Polisi.

"Mtuhumiwa huyu amewekwa kizuizini kutokana na kusambaza taarifa za uongo kuwa binti huyo aliyefanyiwa kitendo cha kikatili kwa kubakwa na kulawitiwa kuwa amekufa.

"Binti huyu yuko hai na si kweli kama mtuhumiwa Lwiza alivyozusha kwenye mitandao ya kijamii. Jeshi la Polisi linaendelea kutoa wito kwa jamii kujiepusha na kutoa taarifa za uongo ambazo hawana uhakika nazo kwani kufanya hivyo ni kosa kisheria," alisema Muliro.

# Ripoti huduma kibingwa yataja magonjwa tishio

**Na Mary Geofrey**

RIPOTI ya Utoaji Huduma za Kibingwa katika hospitali 184 za halmashauri nchini, inaonesha kuwa magonjwa ya shinikizo la juu la damu (BP), ugumba, mfumo wa hewa, moyo kwa watoto na tezi dume yanaongoza.

Aidha, madaktari bingwa wamefanikiwa kufanya upasuaji kwa watoto wa kiume 20 waliokuwa na uume ulioangalia chini, ambao ungesababisha ulemavu wa kudumu.

Pia wamefanya upasuaji wa kundoa mawe kwenye vibofu vya mikojo ikiwamo jiwe la ukubwa wa kilo 1 na gramu 200 na upasuaji wa goita.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa ripoti hiyo ya Mpango Kambambe wa Madaktari Bingwa wa Dk. Samia.

Mpango huo una lengo la kusogeza huduma za kibingwa kwa wananchi, kuimarisha na kuanzisha wodi maalum za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu 'NCU'.

Mpango huo ulianza Mei 6 hadi Juni 8, mwaka huu, na madaktari bingwa wa wanawake na uzazi, watoto, huduma za usingizi na ganzi, magonjwa ya ndani na upasuji na mfumo wa mkojo ambao waliona wagonjwa takribani 70,000.

Ummy alisema kati ya wagonjwa 22,057 wa magonjwa ya ndani walioonwa, shinikizo la juu la damu liliongoza kwa wagonjwa 7,529 (asilimia 34), likifuatiwa na matatizo ya mfumo wa chakula kwa wagonjwa 4,158 (asilimia tisa).

Pia alisema alisema kati ya wagonjwa 18,044 walioonwa na madaktari hao wa magonjwa ya wanawake na uzazi, matatizo ya ugumba yaliongoza kwa wagonjwa 3,810 (asilimia 21), kujifungua 2,529 (asilimia 14) na tatizo la kutokwa na damu nyingi ukeni isivyo kawaida wagonjwa 2,108 sawa na asilimia 12. Ummy pia alisema kati ya watoto 14,466 walioonwa, matatizo ya mfumo wa hewa na moyo yaliongoza kwa kuwa na wagonjwa 2,352 (asilimia 16), uambukizo wagonjwa 2,091 (asilimia 15), upungufu wa damu na selimundu wagonjwa 1,287 (asilimia tisa) na nimonia wagonjwa 1,030 ambao ni asilimia saba.

Alisema kati ya wagonjwa 10,578 walioonwa na madaktari bingwa wa upasuaji, matatizo ya tezi dume yaliongoza kwa wagonjwa 1,568 (asilimia 15) ikifuatiwa na mfumo wa chakula wagonjwa 1,392 (asilimia 13); uvimbe wagonjwa 1,167 (asilimia 11), ajali na mifupa wagonjwa 1,154 (asilimia 11).

Alisema wizara ilishirikiana na vyama vya kitaaluma kama Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi (AGOTA), Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto (PAT), Chama cha Madaktari Bingwa wa Ganzi na Usingizi (SATA), Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani (EMAT) na kwamba zilitumika zaidi ya Sh. bilioni 1.4.

Ummy alisema mikoa 10 iliyoongoza kwa wagonjwa wengi waliojitokeza kuonwa na madaktari bingwa na idadi kwenye mabano ni Tanga (4,410), Mara (3,671), Tabora (3,652), Mtwara (3,540), Mwanza (3,256), Ruvuma (3,253), Mbeya (3,126), Kagera (3,122), Pwani (2,966) na Manyara (2,964).

Alisema pia madakatari bingwa wamewajengea uwezo watoa huduma 4,796 na kati ya hao 2,187 (asilimia 46) ni wauguzi na 1,502 (asilimia 31) ni madaktari na wengine ni wataalam wa maabara na wafamasia.

"Kwa kazi hii imefanikiwa sana; wananchi wamepata huduma, tumepunguza gharama, watoa huduma wamepata mafunzo kazini, wodi maalum nane zimeanzishwa za kuhudumia watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu – NCU.

"Vyumba vya upasuaji vilivyokuwa havijaanza kufanya kazi hasa hospitali mpya vimeanza kufanya kazi, vifaa tiba vipya vimeanza kufanya kazi.

"Tumeona hospitali ambazo hazikuwa na vifaa tiba vya kutosha kufanya upasuaji, uongozi wa hospitali uligharamia kuwapeleka wagonjwa Hospitali za mikoa kwa upasuaji," alisema.

**KUPANDIKIZA MIMBA**

Katika hatua nyingine, Ummy alisema wako katika hatua za mwisho za makubaliano ya bei za kupandikiza mimba kwa mashine maalum (IVF - In vitro Fertilization) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kabla ya kuanza huduma Septemba, mwaka huu.

"Nimeshazungumza na Prof. Mohamed Janabi (Mkurugenzi Mtendaji wa MNH) na wako katika hatua za mwisho, ameshanitajia bei ila nimewaambia waendelee kuangalia namna ya bei kuwa nafuu kulinganisha na hospitali nyingine za binafsi.

"Muhimbili tunatoa huduma na lengo ni kumpa huduma mama anayehitaji mtoto, hivyo bei nayo lazima iwe rafiki na siyo itakayomuumiza mama. Hivyo nadhani tunaenda vizuri na hadi Septemba tutakuwa tumezindua," alisema Ummy.

Tayari serikali imeshakamilisha ununuzi wa mashine za kusaidia upandikizaji mimba zilizogharimu Sh. bilioni moja.



Taka zikiwa zimerundikana katika moja ya maeneo ya Jiji la Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Uzoaji taka ulivyogeuka kitendawili, tishio kwa afya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

HALI ya kukosekana kwa maeneo maalumu kwa ajili ya kukusanyia sambamba na kutokuwapo kwa taasisi rasmi za kuzoa taka katika baadhi ya mitaa jijini Mwanza, imesababisha zisambae ovyo na kutishia afya za wananchi.

Katika maeneo kadhaa ya Jiji la Mwanza, mtu akipita atashuhudia marundo ya taka na hata kudhani kuwa ndiyo madampo au ndio utamaduni uliojengeka katika jiji hilo.

Kwa sasa, taka zimezagaa kwenye makazi ya watu, vyanzo vya maji na barabarani hali inayo hatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo.

Ripoti ya Matokeo ya Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2023 kipengele cha Halmashauri za Majiji na Halmashauri za Manispaa nchini iliyotolewa Mei 10, 2024 na Wizara ya Afya ililitaja Jiji la Mwanza kushika nafasi ya mwisho kati ya majiji sita.

Licha ya jiji hili linaloshika nafasi ya pili kwa ukubwa na uchangiaji wa pato la taifa, Mwanza ilishika nafasi ya mwisho ikiwa na asilimia 57 na alama 71 kati ya 124.

Katika shindano hilo, Jiji la Tanga liliibuka la kwanza kwa asilimia 84 likifuatiwa na Mbeya (asilimia 78), Arusha (asilimia 77), Dar es Salaam (66) na Dodoma asilimia 60.

**WANASEMAJE?**

Nipashe ilifuatilia kwa kina suala hilo na kuzungumza na wananchi, viongozi wa serikali huku wakitaka hatua kali zichukuliwe.

Mkazi wa Mtaa wa Nganza, Deogratius Mahinda, alisema tatizo kubwa katika mitaa yao ni kuzagaa ovyo kwa taka katika mazingira. Taka hizo zinatupwa nyakati za usiku na watu kutokana na kutokuwapo maeneo maalumu ya kukusanyia, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa taasisi, wazabuni wa kukusanya taka katika maeneo ya makazi ya watu.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakichimba mashimo holela katika makazi yao kwa ajili ya kutupa taka, ambayo hujaa muda mfupi na kusababisha kuzagaa katika makazi ya watu.

"Licha ya taka hizo kuwa kero katika mazingira, kadhalika zile ngumu kama plastiki na wakati mvua zikiendelea kunyesha, vyanzo vya maji kikiwamo Ziwa Victoria, husababisha uharibifu wa vyanzo vya maji," alisema Mahinda.

Mahinda anaomba uongozi wa Jiji la Mwanza kuhakikisha unaweka wazabuni wenye nguvu katika kuzoa taka hizo na kuzipeleka katika maeneo ya dampo. Pia anashauri Jiji kutenga vituo maalumu kwa ajili ya ukusanyaji wa taka ili kuwaondolea wananchi kero hiyo inayowaweka hatarini kupata magonjwa ya mlipuko. Anasema awali kulikuwa na mzabuni anayezoa taka kwenye makazi na kuzipeleka katika moja ya vituo vya kukusanyia ambako taka zilikuwa nyingi bila kuondolewa kwa kuwa mtoa huduma alisitisha bila taarifa kwa wananchi.

**"Mkakati huu utajumuisha kuimarisha mtandao wa barabara kuu ili kuunganisha maeneo yote ya uzalishaji na masoko, kupunguza gharama za usafirishaji na kuhakikisha bidhaa ...**

**ATHARI DHAHIRI**

Mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu uliotokea mwanzoni mwa mwaka 2024, Mkoa wa Mwanza ulikuwa wa pili kuripoti ugonjwa huo. Januari 9, kilithibitishwa kifo cha mwananchi mmoja wilayani Magu kilichotokana na ugonjwa huo huku Jiji la Mwanza na Ilemela wakibainika wagonjwa saba na washukiwa 18 wa ugonjwa huo.

Aidha, hali hiyo ilitajwa kuendelea kuwa mbaya katika eneo la Jiji la Mwanza ambako Mganga Mkuu wa Mkoa kwa wakati huo, Thomas Rutachunzibwa, alithibitisha kuwapo kwa wagonjwa 112.

Hali hiyo iliyoibuka kutokana na mvua zilizokuwa zikinyesha kwa wakati huo, inadhihirisha kuwa kwa hali ya sasa ya mazingira kutokuhifadhiwa ipasavyo pindi mvua zitakapoanza kunyesha, kutakuwa na hatari kubwa ya kuibuka tena kwa ugonjwa huo.

Mkazi wa Mtaa wa Silivini, jijini Mwanza, Neema Andrew, anataja hali ya uzoaji taka katika eneo hilo inasimamiwa na mwananchi mmoja mmoja kutokana na utaratibu maalum uliowekwa awali kusitishwa. Anasema wako vijana wanaopewa fedha kwa nyakati za usiku ili kutoa taka hizo katika makazi yao.

Hata hivyo, vijana hao hawana maeneo maalum ya kuzipeleka hivyo kulazimika kuzitupa katika barabara za mitaa, ziwani na hata maeneo mengine ya wazi yasiyokuwa rasmi.

"Hali hii inatuathiri kwa kiasi kikubwa kutokana na taka hizo kuzagaa mitaani ambapo tunao watoto wanaoshinda kwenye maeneo hayo hivyo nao afya zao zinakuwa hatarini pindi wanapochezea taka hizo," anasema.

Oscar Evodius, Mkazi wa Mtaa wa Malimbe, anasema licha ya serikali kutokutoa kipaumbele katika mitaa yao kwa kuweka taratibu maalum juu ya uzoaji taka hizo, bado pia elimu haijaifikia jamii kuhusu athari za utupaji taka ovyo pamoja na makosa ya kufanya hivyo.

Aidha, anaiomba serikali kutazama vyema jiji hilo kwa kufanya uwekezaji hasa kwenye magari pamoja na vifaa vingine muhimu vya kuzoa taka, ili kuweka mazingira salama kwa ajili ya afya za wakazi wa maeneo husika.

"Taka si sehemu ya afya ya binadamu na kama mwananchi hali inaathari kubwa katika afya yangu. Pia mvua zikinyesha kuna hatari zaidi ya kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kama ilivyokuwa mwanzoni mwa mwaka huu," anasema Evodius.

**INAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

## ACT-Wazalendo yapendekeza mwarobaini migogoro ya ardhi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT - Wazalendo kimesema ili kutatua migogoro ya ardhi wakulima na wafugaji, ni lazima kuwe na hatua madhubuti za kisera na kiuwajibikaji kwa serikali na jamii.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, changamoto ya migogoro ya ardhi inazidi kuwa kubwa kiasi cha kuwa tishio kwa amani na utulivu nchini.

Aidha, chama hicho kimependelea mambo manne ambayo ni kusimamia utekelezaji wa mipango wa matumizi bora ya ardhi iliyowekwa na wanavijiji wenyewe kupitia mikutano mikuu ya vijiji.

Pia kimeshauri kukomesha vitendo vya rushwa miongoni mwa viongozi wa serikali za mitaa na vijiji ili kuondoa upendeleo na uporaji wa raslimali ardhi.

Chama hicho kimependekeza pia serikali kutumia majukwaa rasmi kama Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) na Mikoa (RCC) kujadili masuala hayo wa upana na kuwashirikisha wawakilishi wa wakulima na wafugaji ili kujenga maelewano miongoni mwao.

Aidha, ACT-Wazalendo imependekeza serikali kufanya uamuzi wa kisera kuwapa mamlaka wananchi kutoa ridhaa ya uwekezaji ili kuhakikisha kuwa hakuna uwekezaji utakaofanyika kwenye ardhi ya wananchi bila ridhaa ya wananchi wenyewe.

"Katika hili ni muhimu sana kuwezesha wananchi kunufaika na ardhi yao waliyoitoa kwa ajili ya uwekezaji kwa wao kuwa sehemu ya umiliki wa mradi husika kwa mfumo wa ardhi kama mtaji," alisema Semu.

Kiongozi huyo alisema chama hicho kinaamini migogoro ya ardhi inapaswa kupewa uzito mkubwa katika mijadala ya kisera na maamuzi na uongozi.

"Uchambuzi wetu unaonyesha kuwa migogoro hii ipo makundi makuu matatu, migogoro ya wananchi, kati ya wafugaji na wakulima kuhusu maeneo ya kilimo na maeneo ya malisho, nyingine ni kati ya wananchi dhidi ya serikali hususani kuhusu mipaka kati ya vijiji na hifadhi za wanyamapori au misitu.



Bingwa mbobezi wa Watoto wanaohitaji Uangalizi Maalumu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Namala Mkopi, akifurahia jambo na mtoto aliyeruhiwa kwa kukatwa koo na mfanyakazi wa ndani 'house girl', Maliki Hashimu (6), kabla ya kuruhusiwa kutoka hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Siku 13 ICU zilivyookoa maisha ya mtoto aliyekatwa koo na hausigeli

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imeokoa maisha ya mtoto Maliki Hashim (6), aliyejeruhiwa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali kooni, kwa kutumia hatua tano huku akilazwa katika chumba cha uangalizi maalumu (ICU) kwa siku 13.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Hashim Kitumbi, mbali na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kugharamia matibabu ya Maliki, amewaomba wadau na wasamaria wema kuwapa msaada wa kuboresha makazi, ili kumwondolea kumbukumbu mbaya mwanawe kwa kile kilichomtokea.

Bingwa wa Magonjwa na Tiba ya Dharura na Ajali MNH, Dk. Juma Mfinanga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema mtoto huyo alipokewa hospitalini hapo kwa dharura Julai 15, mwaka huu, akiwa na hali mbaya.

"Tulimpokea mtoto huyu na kikosi kizima cha EMD (idara ya dharura) ambao ni madaktari wa magonjwa ya dharura wakiwamo madaktari, wauguzi muda wa saa 3:00 usiku. Aliletwa idara yetu akiwa na wenzetu kutoka hospitali binafsi iliyoko Goba, akiwa na mama yake. Alikuwa na hali mbaya sana.

"Kwanza alikuwa na majeraha makubwa shingoni yalisababishwa na kitu chenye ncha kali na kusababisha njia yake ya kupumulia, yaani mfumo wa hewa, kuwa umekatika kabisa. Alikuwa amekatwa shingoni mbele na nyuma, alivuja damu nyingi," alisema Dk. Mfinanga.

Alisema hatua ya awali iliyochukuliwa na EMD ni kuokoa maisha ya mtoto kwa kuhakikisha anarejeshewa hali ya upumuaji kwa kutafuta kipande cha upumuaji kilichokatwa na kuunganisha na mpira ulioingia hadi kwenye mapafu.

"Tulimwekea mpira na kuuingiza kwenye mashine na baada ya kuona anapumua, hatua ya pili ilikuwa kurejesha kiwango cha damu kilichopotea kisha tukaona mapigo ya moyo yanarejea, anapumua kwa msaada wa mashine halafu tukawaita madaktari bingwa wa mfumo wa masikio, pua na koo (ENT)," alisema.

Dk. Mfinganga ambaye ni Mkuu wa Idara ya Tiba na Magonjwa ya Dharura na Ajali MNH, alisema pia madaktari wa watoto upande wa ICU ya watoto walishirikishwa baada ya hatua hizo tano, huku kikosi hicho kikipanga namna ya kuokoa maisha yake na Maliki kulazwa ICU kwa takribani wiki mbili.

Mkuu wa Idara ya Masikio, Pua na Koo MNH, Dk. Aslam Nkya, ambaye ni bingwa mbobezi wa upasuaji wa shingo, alisema mtoto huyo alifanyiwa urekebishi wa koo, hasa eneo lililojeruhiwa na kitu chenye ncha kali.

"Kitu chenye ncha kali kilitenganisha koo kabisa. Ilikuwa kazi ya kurudishia koo na eneo la nyuma likae vizuri. Kwa kushirikiana na madaktari wa koo, tiba usingizi na wauguzi, tulimpeleka chumba cha upasuaji na kutafuta kifaa na njia nyingine ya kupumulia, anayopumulia hadi sasa inaitwa 'trachestomy'.

"Baada ya hapo tulifanya upasuaji wa kurekebisha na kuunganisha njia ya koo, ili arejee katika hali ya kawaida na kutibu jeraha la nyuma ya shingo ambalo lilikuwa limefika katika mfupa wa nyuma yaani uti wa mgongo," alisema.

Dk. Nkya alisema mtoto huyo kwa kipindi cha wiki mbili, atapumua kwa kutumia kifaa hicho hadi kitakapotolewa na kisha kupumua kama kawaida na kuongea kama ilivyokuwa awali. Bingwa wa Watoto katika Tiba ya Watoto Wanaohitaji Uangalizi Maalumu (Paediatric Intensity) MNH, Dk. Namala Mkopi, alisema Maliki amekaa hospitalini hapo kwa siku zipatazo 24 kati ya hizo 13 akilazwa ICU.

"Tulianza kumwona Maliki akiwa EMD na baada ya hapo alikuja kwetu na kuendelea pale walipoishia wenzetu kwa kusubiri kwanza aendelee kuimarika, kuwa salama na kumwondolea hatari ya kupoteza maisha, ili aendelee na upasuaji mwingine," alisema Dk. Mkopi.

"Tumeshirikiana na wataalamu wa lishe kuhakikisha anapata lishe bora na wanaofanyisha mazoezi wafiziotherapia, ili mtoto aweze kuimarika kusimamisha shingo yake, kutembea na sasa anaweza kula, kuongea, kutembea," alisema bingwa huyo.

Baba mzazi wa mtoto huyo, alimshukuru Rais pamoja na uongozi wa MNH, huku akiomba msaada wa kufanyia marekebisho makazi yao, ili kuwa salama kwa mtoto wake.

"Namshukuru mheshimiwa Rais ametufanyia kazi kubwa sana ya kuokoa maisha ya mtoto wetu pia nawashukuru madaktari waliotupokea tangu siku ya kwanza, Mungu atawalipa na hata wanahabari wote tunawashukuru wamesaidia kuleta msukumo wa jambo hili.

"Kwa sasa hivi naweza kusema tuna kipindi kigumu sana, tulipo ni hospitali ila tuna muda wa kurejea nyumbani lakini pale nyumbani si salama sana na aina ya tukio lililopotokea, nawaomba si tu tumwangalie mheshimiwa Rais, lakini wadau na Watanzania watakaoguswa pale nyumbani kwa haraka, ili kufanyiwa marekebisho.

"Ingekuwa marekebisho ya muda mrefu sisi wenyewe tungejitahidi, ili Maliki akirudi nyumbani aone hapa ndio nilifanyiwa hivi... hali hiyo imwondoke kabisa, tunaomba sana," alisema.

Maliki anadaiwa alijeruhiwa Julai 15, mwaka huu, Goba mkoani Dar es Salaam, sehemu ya koo na hausigeli na taarifa za tukio hilo kuthibitishwa na Jeshi la Polisi Kanda Maalumu Dar es Salaam na Rais Samia akaahidi kulipia gharama za matibabu.

Baada ya tukio hilo, Maliki alifikishwa hospitali MNH-Mloganzila na kisha, kwenda MNH Upanga, kwa ajili ya matibabu zaidi kwa kuwa baada ya kujeruhiwa ilisababisha ashindwe kupumua, kuongea na kupata maumivu na kupoteza damu nyingi.

Wataalamu hao walibaini jeraha la mbele ya shingo, liliharibu tezi la mbele liitwalo (thyroid gland) kwa kulikata katikati na kusababisha mtoto huyo kuvuja damu kwa wingi, kupata maumivu makali kutokana na kukatwa sehemu iitwayo (trachea) ambako hewa inayotoka kwenye mapafu hupita.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa serikali upanuzi wa kiwanda sukari wa kupongezwa

**MAPEMA** mwaka huu, Watanzania walipata adha ya kupanda kwa bei ya sukari. Licha ya kupanda bei, bidhaa hiyo ilikuwa adimu kupatikana kutokana na kuuzwa kwa kificho na hata ilipopatikana, iliuzwa kwa bei kubwa hadi Sh. 8,000 kwa kilo.

Kutokana na kupanda huko, serikali ilifanya kila jitihada kuhakikisha wananchi wanaondokana na adha hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa vibali vya kuagiza nje ya nchi kuziba pengo lililokuwapo.

Jana, Rais Samia alivunja ukimya kuhusu adha hiyo kwa kubainisha kuwa alipata maumivu baada ya kusikia bidhaa hiyo ambayo ni muhimu kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu na viwandani, ikiuzwa kwa bei hiyo takriban mara mbili na nusu ya bei iliyokuwapo awali.

Rais alibainisha kuwa uhaba huo wa sukari ulisababishwa na viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo, kushindwa kufanya uzalishaji kutokana na mvua nyingi zilizonyesha kuanzia Januari hadi Aprili, mwaka huu.

Habari njema ni kwamba Rais ameliona hilo na katika kuonesha dhamira ya kweli kwa wananchi kutokupata adha kwa wakati ujao, ameagiza upanuzi wa kiwanda cha pili cha sukari ya Mkulazi (Mkulazi II) baada ya kile cha awamu ya kwanza, mkoani Morogoro, kilichozinduliwa jana kikiwa kimekamilika kwa kugharimu Sh. bilioni 340. Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Jeshi la Magereza.

Rais Samia, wakati wa uzinduzi huo, aliagiza kuanza kwa ujenzi wa kiwanda kipya cha Mkulazi II ili taifa liwe na uhakika wa chakula hasa sukari baada ya kukamilika na kuanza uzalishaji wa tani 50,000 kwa mwaka kwa Mkulazi I kilichoko Mbigiri, Kilosa mkoani Morogoro.

Rais alisema baada ya kukamilika kwa kiwanda hicho cha pili, uzalishaji wa sukari kwa Mkulazi I na Mkulazi II utafikia tani 70,000 kutoka 50,000 zinazozalishwa sasa, hatua ambayo itawezesha kupunguza pengo kubwa la bidhaa hiyo. Licha ya kuongeza uzalishaji na kuziba pengo la uhaba, Rais Samia alisema hakutakuwa na visingizio vya upungufu wa sukari mvua ikinyesha kwa kuwa viwanda hivyo vya serikali vitakuwa vikiendelea na uzalishaji.

Kwa ujumla, hatua hiyo ya serikali ya kuongeza kiwanda kingine cha sukari, ni ya kupongezwa kwa sababu imeona kwa kina wananchi waliopata adha wakati bidhaa hiyo ilipoadimika na kununua bei ya kuruka. Vioja hivyo vya wafanyabiashara vya kuficha sukari kila kunapokuwa na uzalishaji kidogo vitafikia tamati.


Licha ya hiyo, viwanda hivyo vitawezesha kupatikana kwa ajira kwa vijana ambao kilio hicho kimekuwapo muda mrefu na hata kuonekana sawa na donda ndugu lisilipata tiba mujarabu.

Pamoja na pongezi hizo, ni wakati mwafaka kwa serikali kujifunza kuhusu kuporomoka na kufa kwa viwanda na mashirika ya umma kulikosababisha wafanyakazi wengi kupunguzwa kazi na wengine kukosa stahiki zao.

Katika kujifunza huko, serikali inapaswa kujiondoa kwenye uendeshaji wa kila siku wa viwanda hivyo na kuweka menejimenti yenye uwezo na itakayooongoza taasisi kwa ufanisi na weledi. Serikali kazi yake inapaswa kuwa na bodi imara ya wakurugenzi itakayosimamia sera na miongozi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Ni dhahiri kwamba kama ilivyo kwa msemo kwamba usiangalie ulipoangukia bali ulipojikwaa. Serikali itafanya hivyo kwa ustawi wa viwanda hivyo vya sukari na hatimaye kuleta tija na kuwaondolea Watanzania adha ya ukosefu wa sukari.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tahadhari dhidi ya homa ya nyani

Na Moshi Lusonzo

**KAMA** mataifa jirani ikiwamo Kenya yamethibitisha kuwa na wagonjwa wa homa ya nyani maarufu kama monkey pox au 'Mpox' Tanzania, sisi ni nani tusichukue tahadhari?

Katika taarifa inayotolewa na Wizara ya Afya ya Kenya, mgonjwa mmoja amegundulika Mombasa eneo linalopakana na Tanzania upande wa Kusini Mashariki.

Tayari ugonjwa huo umeripotiwa kusambaa kwa kasi huko Congo (DRC), Rwanda, Burundi na Afrika ya Kati.

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO) limetoa tahadhari ya kuibuka kwa virusi vipya vya homa hiyo kali ambayo tayari imeua idadi kubwa ya watu nchini DRC.

Kutokana na ugonjwa huo kuenea kwa kasi kutoka taifa moja hadi lingine, serikali ya Tanzania inatakiwa kutambua kuwa, ugonjwa huo umepiga hodi na kunahitajika jitihada za kuzuia kuingia nchini ili kuepusha kutokea kwa madhara yanayotokana na ugonjwa huo kama inavyotokea mataifa jirani.

Inaelezwa kuwa, ugonjwa huo unaambukizwa kwa kugusa majimaji kutoka kwa mtu anayeugua au kuambukizwa, hivyo ni rahisi kusambaa endapo watu hawatachukua tahadhari za kujilinda ikiwamo kunawa mikono.

Kama tayari Kenya na Uganda zimeripoti kuwapo kwa maambukizi hayo, hivyo ni rahisi kuingia nchini kutokana na mwingiliano baina ya Watanzania na watu nchi hizo. Hii inatokana na sababu mbalimbali hasa shughuli hasa za kiuchumi na kijamii.

Aidha, Wizara ya Afya ina wajibu wa kuwaelimisha watu jinsi ya kujilinda na ugonjwa huo kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari, vipeperushi na kuweka matangazo mtaani.

Pamoja na serikali kueleza kuwa ipo makini na ugonjwa huo, lakini inatakiwa kufanya juhudi zaidi kwa kuwapeleka maofisa wa afya katika maeneo ya mipakani, vijijini na katika miji ya mipakani kuwapa elimu wananchi ambao hawana ufahamu wa maradhi hayo.

Homa ya nyani, ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya nyani na dalili zake ni pamoja na kutokwa damu'

Licha ya ugonjwa huo kuenea kwa njia ya kama vile kugusana moja kwa moja na mtu iliyeambukizwa, majimaji ya mwili kama damu, jasho, mate na haja ndogo si kitu cha kupuuzwa.

Inaelezwa kuwa, unaweza kuambukizwa kupitia mate mtu anapokohoa hivyo tahadhari ni muhimu.

Dalili kubwa ni mtu kupata upele kwenye ngozi, vidonda mdomoni na sehemu za siri.

Hata hivyo, Mpox hutibika bila ya matatizo ndani ya wiki mbili hadi nne.

Pamoja na ugonjwa huo kuwa na tiba, serikali kupitia wizara mbalimbali ingeendesha zoezi la kutoa chanjo kwa watu wanaoishi katika maeneo yanayotiliwa shaka hasa mipakani.

Kama tulivyovuka salama katika janga la UVIKO-19, baada ya elimu ya kutosha kutolewa pamoja na kutoa chanjo, ni wazi hata kwa ugonjwa huu serikali inaweza kupambana na hatimaye ukaishia nje ya mipaka yetu.

Pia, vitengwe vituo maalumu vya kutolea matibabu kama ilivyo kwa magonjwa mengine ya mlipuko, pamoja na kuujulisha umma mahali vilipo ili patakapotokea tatizo hilo iwe rahisi kukimbilia.

Mathalani, katika maeneo ya mipakani, viwanja vya ndege na vituo vya mabasi, kuwapo na vipimo vya kuangalia viwango vya joto kwa watu wanaotoka katika nchi zilizothibitisha kuwapo kwa ugonjwa huo nchini mwao.

Serikali iweke mkakati maalumu kwa kuwatambua watu wanaovuka mipaka kwa njia haramu, hivyo njia hii itafaulu kama watashirikishwa viongozi wa serikali, kidini na kisiasa katika kuwaelemisha wananchi.

Kwa upande wa wananchi nao wanawajibu kufuata yale yanayoelezwa kutoka vyanzo muhimu vya afya, na tuache masuala ya kupuuzia kwani akipata mtu mmoja basi atayaweka hatarini maisha ya watu wengi.

Tuache tabia ya kuwahudumia watu wenye matatizo kabla ya kuwafikisha hospitali. Ukipata mgeni mwenye tatizo linaloambatana na dalili za homa ya nyani, ni muhimu kumuwahisha hospitali, badala ya kumpatia matibabu nyumbani.

Kwani kwa kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha ya watu wengine na kuliingiza taifa kwenye janga kutokana na kupuuza maelekezo.

Tunaipongeza serikali kwa kutoa taarifa mapema kuhusu maendeleo ya ugonjwa huo katika nchi za jirani kwani hatua hiyo imewafanya watu kuwa na tahadhari.

Taarifa kama hizo ziendelee kupatikana kila mara ili kuwafanya watu kupata habari sahihi na kwa wakati kuhusu ugonjwa huo.

Kufaulu kuepukana na ugonjwa huu hatari kutatokana na ushirikiano kati ya serikali na wananchi.

Waswahili wanasema 'kinga ni bora kuko tiba', hivyo wote tushikamane tujilinde dhidi ya ugonjwa huu badala ya kuhangaikia tiba ambayo ni gharama kwetu sote.

# Gesi asilia kutumika kuzalisha mbolea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amesema serikali kupitia wizara hiyo iko katika hatua za mwisho za mazungumzo na wadau ili kuanza uzalishaji wa mbolea kwa kutumia gesi asilia.

Mhandisi Mramba amesema hali itakayosaidia kupunguza uingizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Mramba alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo maarufu kama Nanenane yanayofanyika viwanja vya Nzuguni, jijini hapa.

Alisema nishati ni wadau wakubwa katika kuwezesha shughuli za kilimo na ufugaji nchini, ndiyo maana wameona hiyo ni fursa nyingine katika maendeleo ya sekta hizo hasa kutumia gesi asilia kuzalisha mbolea.

Katibu mkuu huyo alisema uzalishaji huo ukianza, utasaidia wakulima kupata mbolea kwa gharama nafuu na kuipunguzia mzigo serikali kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Pia alisema Wizara ya Nishati imeshiriki maonesho hayo kutokana na kuwa na jukumu kubwa la kupeleka huduma za umeme kwenye miradi ya umwagiliaji na viwanda vidogo vya kilimo.

“Lakini hivi sasa tunafanya jitihada kuongeza upatikanaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya moto ili kuwezesha kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo na mifugo.

“Sasa hivi magari ya kampuni ya Dangote ndiyo yanatumia gesi asilia lakini na sisi kama serikali tunafanya jitihada za makusudi kuongeza upatikanaji wa gesi kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya moto ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo na mifugo,” alisema. Mramba pia alisema maonesho hayo ya Nanenane watayatumia kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwamo matumizi ya gesi itokanayo na kinyesi cha mifugo.

“Tunakwenda kuhamasisha watu wenye mifugo kuanza kutumia nishati itokanayo na kinyesi cha mifugo (biogas), hata kama mtu na ng’ombe wawili basi hao watumike kuzalisha nishati safi ya kupikia,” alisema.

Pia alisema tayari wameandaa mkakati wa kuelimisha jamii umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ambao utekelezaji wake unaanza mwishoni mwa mwezi huu.

“Kupitia mkakati huu, tunakwenda kutoa elimu kwa umma pamoja na kugawa mitungi ya gesi ya kupikia na tayari Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wameshaingia makubaliano na magereza yote nchini kuwafungia mitungi,” alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investments (WHI), Dk. Fred Msemwa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano mkuu wa kwanza wa mwaka wa Mfuko wa Uwekezaji Faida (Faida Fund), unaotarajiwa kufanyika Jumamosi ijayo katika jiji hilo. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uwekezaji wa WHI, Paskali Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau wabainisha changamoto kwa vijana kuelekea uchaguzi

**Na Maulid Mmbaga**

WATAFITI wa masuala ya kisiasa wamebainisha kuwa changamoto za kiuchumi, mila na desturi potofu ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili vijana na wanawake na kusababisha wasichaguliwe katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Hayo yanabainishwa ikiwa imebaki miezi kadhaa kuelekea uchaguzi mdogo wa serikali za mitaa Novemba mwaka huu na uchaguzi mkuu Oktoba mwakani.

Katika kuwaandaa vijana kushika nafasi za uongozi, asasi isiyo ya kiserikali ya ENVIROCARE inaendesha programu maalumu kwa ajili ya kuhamasisha vijana na wanawake kujitokeza kugombea pamoja na kuwaongezea uelewa wa namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Akizungumza na gazeti hili jana Dar es Salaam, Meneja wa Mradi wa Uhamasishaji Wanawake na Vijana kushiriki katika kugombea nafasi za uongozi kutoka ENVIROCARE, Godlisten Muro, alisema katika utafiti wao walibaini uchaguzi unatawaliwa na rushwa na ambazo zinatolewa na wenye hali nzuri kiuchumi.

**“Pia kuna suala la rushwa ya ngono hasa kwa wanawake na wasichana. Ili kushika nafasi mbalimbali za uongozi inabidi watoe rushwa ya ngono.**

“Pia kuna suala la rushwa ya ngono hasa kwa wanawake na wasichana. Ili kushika nafasi mbalimbali za uongozi inabidi watoe rushwa ya ngono. Sasa hivi ni vitu ambavyo ni vikwazo kwa vijana, na vinakwamisha wengi kushika nyadhifa hizo,” alisema Muro.

Aliongeza kuwa wamebaini watu wengi wanaamini kuwa vijana na wanawake hawafai kuwa viongozi, wakidhani kigezo cha uzee ni kuwa na busara na kwamba hizo ni mila na desturi potofu ambazo zinapaswa kukemewa katika jamii.

Pia alisema sababu hizo ziliwalazimu kufikiria kutoa elimu kwa vijana kitoka vyama mbalimbali ikiwamo kujua sheria mbalimbali za uchaguzi, na kwamba wanaamini uelewa watakaoupata utawawezesha kugombea nyadhifa mbalimbali bila vikwazo.

“Vijana wanapaswa kuamua mustakabali wa taifa na vyama vyao vya kisiasa, wawe na ujasiri, wasiogope, wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi na wajiamini. Pia, niisihi jamii kuondokana na kasumba ya kwamba vijana hawawezi, popote duniani wanaoleta maendeleo ni vijana, wanauwezo wa kuleta mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa,” alisema Muro.

Ofisa kutoka Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), Janeth Kweka, alisema mafunzo waliyopatiwa yamewasaidia kujua umuhimu wa kushiriki chaguzi, akieleza kuwa kikwazo kikubwa kwa vijana wengi ni uoga kutokana na kutokuwa na kipato, akitoa wito kwa wanawake kwamba ni wakati wao wa kuonesha wanaweza.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA) wilaya ya Ilala, Dedan Wangwe, alisema ana matumaini makubwa kwamba uelewa alioupata utamjenga na kumpa matokeo kuelekea uchaguzi unaotarajiwa kufanyika siku chache zijazo, kwa kuwa anatamani kuwania katika nafasi mojawapo ya uongozi.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Vijana wanaojitolea kupewa kipaumbele ajira

**Na Lusungu Helela,** SUMBAWANGA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amesema serikali inaandaa utaratibu rasmi wa kutambua mchango wa vijana wanaojitolea kwenye taasisi mbalimbali za serikali huku akiwataka vijana hao kuwa wavumilivu na wasikatishwe tamaa.

Amesema utaratibu huo utasaidia kupata watu sahihi wanaojitolea badala ya mamluki ambao hupenyezwa na ndugu pindi fursa za ajira zinapojitokeza.

Sangu alisema hayo juzi kwa nyakati tofauti katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata za Ikozi na Kalambanzite, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kwanza tangu alipouteliwa kushika wadhifa huo.

Alisema udanganyifu huo umekuwa ukifanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu wenye ndugu zao na kusababisha manung'uniko kwa vijana sahihi wanaojitolea

Kutokana na hali hiyo, Sangu alisema serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iko katika hatua ya mwisho ya kuandaa utaratibu ambao utakuwa mwarobaini wa namna bora wa kutambua mchango wa vijana hao.

Katika hatua nyingine, Sangu alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo kusababisha baadhi ya watumishi ambao si waaminifu kuanza kufuja fedha hizo. Hatua hiyo imesababisha Sangu kuielekeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwabana watumishi hao ili kukomesha tabia hiyo.

Hata hivyo, alisema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuwasimamia watumishi wote nchini ili kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinapopelekwa, zinasimamiwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa

"TAKUKURU hakikisheni mnawabana watumishi ambao ni wadokozi wa fedha za miradi ya maendeleo inayotolewa na Rais wetu," alisisitiza Sangu.




Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi rasmi wa mashindano ya Kimataifa ya Qur'an Tukufu kwa wasichana unaotarajiwa kufanyika Agosti 31, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MIRAJI MSALA**




# Miradi 15 kutekelezwa mageuzi ya kilimo nchini

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

OFISI ya Mabadiliko ya Kilimo (ATO), imejipanga kutekeleza miradi 15 tofauti kwa lengo la kuleta mapinduzi chanya ya kilimo nchini.

Pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo, ATO pia inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Mageuzi ya Kilimo (AMP) ambao unatoa mtazamo wa kubadilisha mifumo ya chakula ya Tanzania ifikapo mwaka 2050, ikiwa na mipango ya vitendo kwa mwaka 2030.

Akizungumza jana jijini Dodoma kwenye maonyesho ya 31 ya Kimataifa ya Kilimo na Mifugo, maarufu kama 'Nanenane ", Mkurugenzi Mtendaji wa ATO, Elizabeth Missokia, alisema malengo makuu ya kimkakati ya AMP ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa bidhaa muhimu hadi kufikia asilimia 50.

Pia kuongeza kipato cha mkulima mdogo kwa asilimia 20, pamoja na kuhamasisha maendeleo ya biashara 1000 za kati na kubwa katika mnyororo mzima wa thamani.

"Mkakati huu pia unalenga kuwezesha mauzo ya bidhaa za nje na kuweka mazingira wezeshi kwa wakulima ili kuendana na Dira ya Tanzania ya 2050," alisema.

Alisema ATO imeainisha, na inatarajia kutekeleza miradi 15 ili kutatua vizuizi muhimu katika mnyororo wa thamani wa kilimo.

"Miradi hii inazingatia kuongeza maeneo ya umwagiliaji, kuboresha uzalishaji wa mbegu, kuongeza afya ya udongo, na kuimarisha uwezo wa usindikaji na usafirishaji, miongoni mwa mengine," alisema.

Alisema ofisi hiyo inajikita katika kuisaidia serikali kutimiza malengo ya kati ya mwaka 2030, ikiwa ni pamoja na kufikia kiwango cha ukuaji wa asilimia 10 kila mwaka katika kilimo, kuimarisha uzalishaji kwa zaidi ya asilimia 50, na kuongeza mapato ya wakulima wadogo kwa zaidi ya asilimia 25.

"Pamoja na mambo mengine, ATO imejizatiti katika kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo nchini Tanzania kwa kuwa shirikishi kwa wadau wote wa kilimo ili kuongeza uchumi wa mkulima mdogo na kuongeza pato la taifa," aliongeza.

Ofisi ya ATO iliyoundwa ikijumuisha Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuratibu mchakato wa mabadiliko ya kilimo nchini. Ofisi hiyo ilizinduliwa na Waziri wa Kilimo na Mkurugenzi wa AATI wakati wa kilele cha Mifumo ya Chakula Afrika iliyofanyika Dar es Salaam mwaka 2023.

Uasisi wa ofisi hiyo ulitokana na maazimio yaliyowekwa na wakuu wa nchi za Afrika kwenye Mkutano wa Mifumo ya Chakula, Dakar nchini Senegal.

Kwenye mkutano huo pia uliazimia kuundwa kwa Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo na Chakula ambalo litakuwa na jukumu la kumshauri Rais kwenye masuala yote yanayohusu kilimo na chakula. ATO itakuwa inatoa usaidizi wa kitaalamu kwenye baraza hilo.



# Kampuni 2,000 kutopewa zabuni serikalini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KAMPUNI zaidi ya 2,000 hazitapewa zabuni serikalini baada ya kubainika taarifa zao kutosajiliwa katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Michael Moshiro, wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwazi na Uwajibikaji (ITAC) 2024, jijini Arusha.

Akiwasilisha mada kuhusu teknolojia inavyochochea uwazi katika ununuzi, Moshiro alisema kuwa walibaini baadhi ya kampuni zina shida katika usajili baada ya kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha mifumo ya serikali inasomana.

Alisema mfumo wa NeST umetengenezwa na vijana wa kitanzania na kwamba hadi sasa jumla ya taasisi 26,000 zinatumia mfumo wa NeST kwa simu, zikijumuisha shule na vituo vya kutolea huduma za afya.

Moshiro alisema lengo la kuanzisha mfumo huo ni kutatua changamoto zilizokuwapo katika mifumo iliyopita, akidokeza kuwa thamani ya fedha sasa inaonekana, akiitolea mfano Shule ya Sekondari Msalato, mkoani Dodoma, ambayo hivi karibuni ilitangaza zabuni ya kupatiwa chakula kwa Sh. milioni 52, lakini akapatikana mzabuni aliyetoa huduma hiyo kwa Sh. milioni 39, hivyo kuokoa Sh. milioni 13.

Moshiro pia alisema wamebaini kuwapo baadhi ya viongozi wa kampuni wanaofanya udanganyifu kwamba kampuni zao ni za makundi maalum ilhali siyo kweli. "Kuna mzee mmoja alisajili kampuni yake kwamba ni ya kundi maalum. Alipoambiwa kwamba makundi maalum yanajumuisha wanawake na yanapewa kipaumbele katika zabuni za serikali, aliamua kuisajili kampuni kwa jina la mkewe, huku binti yake naye akijumuishwa kuwa sehemu ya viongozi wa kampuni," alisema.


**"Kuna mzee mmoja alisajili kampuni yake kwamba ni ya kundi maalum. Alipoambiwa kwamba makundi maalum yanajumuisha wanawake na yanapewa...**

Hata hivyo, alisema mfumo huo na mingine siyo suluhisho dhidi ya vitendo vya rushwa; vita dhidi ya rushwa inapaswa kuanzia katika nafsi ya mtu na kumjenga kimaadili.

Akichangia kuhusu mada hiyo, Dk. Byaruhanga Aloysius kutoka Uganda, alisema Tanzania imepiga hatua kimifumo kukabiliana na vitendo vya rushwa katika utoaji zabuni serikalini na kwamba hali ni mbaya kwao Uganda katika eneo hilo na zabuni na ununuzi serikalini.

"Tunajifunza kutoka kwenu Watanzania. Huu mfumo wa NeST ni mzuri sana. Tatizo la nchi zetu za Afrika Mashariki ni rushwa. Rwanda imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti rushwa, nchini kwangu (Uganda) bado tuna hali mbaya," alisema.

Mkutano huo wa siku mbili uliohitimishwa jana, uliandaliwa na Taasisi ya WAJIBU inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu. Taasisi hiyo imeandaa mkutano huo kwa miaka minne mfululizo, mwaka huu washiriki wakijikita kumulika ununuzi wa umma.




Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jesca Nyaki (wa pili kulia), akikabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo maalumu ya ujasiriamali na matumizi ya mifumo ya kidijitali kwa Sylivia Chama, yaliyotolewa kwa vijana wa makundi maalumu na Shirika lisilo la Kiserikali la Digital Opportunity Trust Tanzania (DOT-Tanzania) kwa kushirikiana na Shirika la Songambele Initiative, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. Wengine ni Mwakilishi wa DOT-Tanzania, Denish Otieno (kulia) na wadau wengine. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wanane mbaroni tuhuma matumizi vipimo batili

**Na Allan Isack,** BABATI

WAFANYABIASHARA wanane wa mjini Babati mkoani Manyara, wanaodaiwa kutumia vipimo batili wamekamatwa na Wakala wa Vipimo (WMA) wakati wakifanya biashara ya kuhudumia wateja wao.

Meneja wa Wakala wa Vipimo mkoani Manyara, Denis Misango, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema wamefanya kazi hiyo kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kwenye msako wa kuondoa vipimo batili katika masoko ya mji huo.

"Kwa hapa kwenye mji wa Babati, tumefanya msako mkali na wakushtukiza ambapo wafanyabiashara nane wanaofanya biashara ya kuuza mazao mbalimbali katika masoko hayo, wamekamatwa na kutozwa faini," alisema Misango.

Alisema msako wa kuondoa vipimo batili kwa wafanyabiashara ambao wamekaidi agizo la kutumia mizani za kupimia bidhaa mbalimbali katika masoko ya mji wa Babati unaendelea kufanywa na wakala hao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Misango alisema operesheni hiyo ilianza Julai 18 mwaka huu kwa kutoa elimu kuhusu matumizi ya mizani za kupimia bidhaa zao na waliwataka kuachana na kutumia vipimo batili kama makopo, magunia na madebe.

Hata hivyo alisema kuwa msako huo wa kuondoa vipimo batili kwa wafanyabiashara unaendelea kwa kuwa ni suala endelevu hadi hapo watakapohakikisha sheria inafuatwa.

"Ninawataka wafanyabiashara wote mkoani Manyara ambao wanaendelea kutumia vipimo batili kuacha mara moja kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume na sheria," alisema Misango.

Mfanyabiashara wa mazao wa Soko Mjinga Babati, Ally Juma, amewaomba wakala hao wa vipimo kuendelea kutoa elimu kwao kabla ya kufanya ukamataji huo.

"Tunapaswa kupewa elimu endelevu juu ya matumizi ya vipimo hivyo kwa kuwa sisi tumezoea kutumia vipimo vya magunia na madebe tangu enzi na enzi badala ya mizani," alisema.

Mkazi wa Babati kutoka Mtaa wa Riziki Road, Magdalena Julius, alisema amefurahishwa na msako huo kwa kuwa wafanyabiashara hao wamekuwa wakitumia vipimo hivyo ambavyo siyo sahihi.

Alisema: "Hata watu wa buchani nao wanapaswa kuangaliwa mara kwa mara kwa kuwa mizani wanazotumia kupimia nyama mara nyingine wanazifanyia hujuma".

# DC aagiza viongozi kutumia sensa katika mipango

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MKUU wa Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, Raymond Mangwala, ameagiza viongozi kuanzia ngazi ya wilaya hadi vitongoji kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022, kufanya tathmini ya hali halisi ya maendeleo pamoja na kujiwekea mipango ya baadaye.

Alisema hayo jana wakati wa mafunzo ya usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya sensa kwa viongozi wa dini, wa kisiasa, watendaji serikalini na wadau wa maendeleo wilayani hapa yaliyofanyika katika Shule ya Sekondari Mashati.

Mangwala alisema mafunzo hayo yana umuhimu wa kipekee katika kuongeza kasi ya utendaji kazi wa kila siku kwa viongozi na watumishi wa serikali.

Hata hivyo alisema kwa viongozi mafunzo yatawasaidia kuwajengea uwezo wa kufanya uamuzi bora wenye staha na yatatoa mwanga wa kufahamu walipotoka walipo na wanakokwenda.

"Kwa matokeo hayo yataonyesha idadi ya wazee, vijana, watoto na watu wenye ulemavu walioko katika wilaya yetu na kujua namna gani ya kupeleka miradi ya maendeleo kwa usawa, pamoja na kuchambua hoja mbalimbali zitakazoletwa mezani kwetu," alisema.

Awali akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Meneja Takwimu Mkoa wa Kilimanjaro, Albert Kurwa, alisema mafunzo hayo yatasaidia jamii kutambua vyema matokeo na kuyafanyia kazi katika maeneo yao ya utawala.

Alisema: "Wakati wa uzinduzi Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, alitutaka mbali na kutoa matokeo, pia kuwaelimisha wananchi na viongozi wote namna ya kuyatumia ili yalete tija".

Mbunge wa Rombo, Prof. Adolf Mkenda, alisema ujio wa mafunzo hayo kwa viongozi wa makundi hayo yatasaidia kupunguza ubaguzi hasa utoaji wa rasilimali na miradi ya maendeleo.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa Kilimanjaro, Jackson Masaka aliwataka viongozi kutumia matokeo ya sensa katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika maeneo yao ya utawala.





# Wakimbizi Nyarugusu watakiwa kurudi kwao

**Na Vitus Audax**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Maendeleo ya Jamii na Usalama wa Raia wa Burundi, Brigedia Jenerali Nibona Bonansize, wamewaasa wakimbizi katika Kambi ya Nyarugusu mkoani Kigoma kurudi kwao.

Walisema kwa sasa hali ya kiusalama ni nzuri ukilinganisha na hapo awali.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wakizungumza na wakimbizi kutoka Burundi waishio katika kambi hiyo, ambapo Naibu Waziri Sillo aliwataka kujiandikisha kwa hiari kurudi nyumbani kwao.

Alisema serikali inatambua kuwa, Burundi ina amani na hivyo hawaoni sababu ya kutojiandikisha na kurudi nchini kwao kwa hiari ili kuungana na familia zao kwa ajili ya kulijenga taifa lao.

Naibu Waziri Brigedia Jenerali Bonansize alisema nchi hiyo inawahitaji wakimbizi wote warudi nyumbani ili kuijenga taifa, huku akiishukuru serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuwahifadhi ndugu zao kwa muda mrefu.

Mkuu wa kambi hiyo, Siasa Manjenje alisema kambi hiyo ina wakimbizi 134,920, huku wanaotoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakiwa 87,190 na Burundi 47,588.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, 2024 wakimbizi 1655 wamerejeshwa Burundi kwa hiari ikiwa ni idadi ndogo nje ya malengo ya kurejesha wakimbizi 28,000 katika kipindi cha miezi saba.

# Wajasiriamali 'watokomea' na mabilioni ya halmashauri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama, imevitaka vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kufanya marejesho ya mikopo inayodaiwa, ili kuepuka hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao. Bado vikundi hivyo vinadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.1.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Robert Kwela alibainisha haya juzi ofisini kwake na kueleza kuwa wamejipanga kuhakikisha vikundi vyote vinavyodaiwa vinafanya marejesho kabla ya kuanza kuvitembelea.

Alisema tangu mwaka 2017/18 mpaka April mwaka jana serikali ilipotangaza kusitisha utoaji wa mikopo hiyo walikuwa wameshatoa mikopo ya Sh.bilioni tano kwa vikundi hivyo, ambapo kati ya fedha hizo zaidi ya Sh.bilioni 1.1 hazijarejeshwa.

Robert alisema kwa hatua wanazoendelea kuzichukua wanatarajia ifikapo Oktoba mwaka huu zitakuwa zimerejeshwa zote na kuvipatia fursa vikundi vingine kukopeshwa. "Vikundi vyote vilivyokopa fedha hii vinafahamika kwa kila mwanachama mmoja mmoja kwa sababu fomu zao ziliambatana na picha ndogo, vipo vilivyosambaratika lakini viongozi wake wameendelea kukamatana na kufanya marejesho yake na kila mwezi tunakusanya Sh.milioni 52 mpaka Sh. milioni 55," alisema Kwela.

> **"Vikundi vyote vilivyokopa fedha hii vinafahamika kwa kila mwanachama mmoja mmoja kwa sababu fomu zao ziliambatana na picha ndogo, vipo vilivyosambaratika lakini...."**

Mkazi wa Kata ya Nyahanga, Antony Alphonce aliishauri serikali kuvichukulia hatua za kinidhamu vikundi vyote vya ujasiriamali vilivyotumia fedha hizo kinyume na malengo waliyokuwa wamejiwekea katika kukuza mitaji, kiuchumi na kuondokana na utegemezi.

Naye, Safina Juma alisema ucheleweshaji wa urejeshaji wa fedha za mikopo hizo ndiyo chanzo cha baadhi ya vikundi kukosa mikopo mpaka ilipositishwa April mwaka jana.

Alisema wengi walilazimika kuingia kwenye mikopo umiza ambayo dhamana yake ni samani za ndani ili kukuza mitaji yao na baadhi yao waliishia kufirisiwa.

Alisema katika utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo unaoanza hivi karibuni ni vema wakaweka masharti ya kuwabana watakaoshindwa kulipa kwa wakati ili kutoendelea kupoteza fedha za umma ambazo zimetolewa mahusus kwa ajili ya kuwainua wajasiriamali.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (katikati), akipokea kofia ngumu kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wa pili kushoto), wakati wa hafla ya uzinduzi wa maboresho ya huduma za benki hiyo kwa makandarasi, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi Geofrey Mkinga, (wa pili kulia) ni Meneja wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi Kanda ya Mashariki, Mhandisi Ally Mwita na Meneja wa benki hiyo Kanda ya Dar es Salaam, Seka Urio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yawaonya madiwani wanaokwamisha maendeleo

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza kimekemea vitendo vya baadhi ya madiwani kukwamisha shughuli za maendeleo katika maeneo yao kwa sababu za kisiasa, kwamba hakitawavumilia.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilemela, Yusuph Ernest katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa.

Baraza hilo lilikutana kwa lengo la kumchagua Diwani wa Kata ya Buzuruga Manusura Lusigaliye kuwa Naibu Mstahiki Meya kwa kipindi cha mwaka 2024/25.

Aidha, aliwataka madiwani hao kushirikiana katika shughuli zote za kimaendeleo pamoja na kutekeleza ilani ya CCM ili shughuli za KImaendeleo ziweze kusonga mbele.

Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo, Renatus Mulunga alimpongeza diwani huyo kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo kwa awamu nyingine, huku akiwakata madiwani wenzake kumuunga mkono na kupendana ili shughuli za maendeleo ndani ya manispaa hiyo ziweze kufanikiwa na kuyafikia malengo.

Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Manusura Lusigaliye licha ya kulishukuru baraza hilo kwa kumuamini na kumchagua tena aliwahakikishia ushirikiano pamoja na kuahidi kusimamia fedha zote za maendeleo zitakazoletwa na serikali kuu pamoja na zile za mapato ya ndani.

# TAKUKURU yarejesha mil.4/- za TASAF zilizoibwa

**Na Restuta Damian,** KAGERA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera imerudisha Sh. milioni 4.3 ambazo zilitakiwa kulipa wanufaika 139 wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kijiji cha Kumtama Wilaya ya Ngara mkoani Kagera.

Hayo yamesemwa juzi na Naibu Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Ezekia Sinkala wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu.

Sinkala alisema, fedha hizo zilichukukiwa na wasimamizi wa uhaulishaji wa fedha za TASAF kwa kipindi cha Mei, Juni, Julai na Agosti ikiwa ni mgao wa wanufaika hao kwa awamu mbili.

Alisema taarifa za ubadhirifu huo, zilibainikaa katika mkutano wa hadhara uliokuwa wa kutatua kero za wananchi wanaonufaika na mpango huo.

"Katika ufuatiliaji ilibainika kwamba fedha husika kwa malipo ya awamu zote mbili katika Kijiji cha Kumtama ilikuwa Sh. milioni 9.3 yaani fedha ya awamu ya kwanza ilikuwa Sh. milioni 4.6 lakini kwa makusudi wasimamizi walitumia uelewa mdogo wa wanufaika kuwaibia fedha hizo,"alisema Sinkala.

Aidha, alisema baada ya kufanyiwa mahojiano wasimamizi hao ambapo ni watumishi wawili wa Halmashauri ya Ngara, Mtendaji wa Kata, Mwenye Kiti wa Kitongoji, Mwenye Kiti wa Kijiji walikiri kuchukua fedha hizo na kuahidi kurudisha.

Alisema wasimamizi hao walirejesha sehemu ya fedha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na fedha hizo zilirejeshwa kwa wananchi ambao ni wanufaika.

ALHAMISI AGOSTI 8, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Kukausha dagaa juani na mwambani sasa basi, iko nyumba inayotumia jua na gesi**




Ukurasa 13

PMI na mkakati kutokomeza malaria



Ukurasa 14

**Baba pombe unazokunywa ni hatari**

AFYA

# TASAF ilivyomaliza vilio kuzika kila uchao, ilipojenga hospitali

**Na Restuta James**



Meneja Miradi TASAF, Paul Kijazi, akielezea taarifa za kituo cha afya Bwawani. **PICHA: RESTUTA JAMES**

UKIFIKA katika kijiji cha Themi ya Simba, kilichoko Kata ya Bwawani mkoani Arusha, unapokelewa na historia za kusikitisha.

Wakazi wanaeleza walivyopoteza ndugu wakiwapeleka hospitali kwa kuwabeba mgongoni, machela au kutumia mikokoteni ya ng'ombe. Ni simanzi, wengine wanakumbuka walivyofiwa na mama, mtoto au mke, wajawazito na watoto kama anavyosimulia Margaret Jonas, aliyempoteza baba mzazi wakimwahisha kituo cha afya Nduruma, kilichopo kilometa 10 kutoka nyumbani kwao kijijini Themi ya Simba.

Kukosekana barabara na kituo cha afya kinawafanya wakazi wa Bwawani kuwa jamii 'iliyotengwa', hasa nyakati za mvua. Kwenye kiangazi kutembea umbali mrefu kufikia huduma za afya ni changamoto.

"Barabara yetu haipitiki wakati wa mvua, mgonjwa anabebwa mgongoni au na tela la ng'ombe, ndiyo maana tumepoteza ndugu zetu kukiwapeleka Nduruma au kwenye rufaa Arusha ambako ni kilometa 50 kutoka Theme.

"Kipindi cha mvua pikipiki hazipiti wala gari, mgonjwa anabebwa na tela la ng'ombe. Tunaomba serikali itufungulie zahanati haraka kwa sababu watu wanaendelea kufa," anasema Margret.

Aisha Mshangai anaeleza namna alivyonusurika kifo akienda kujifungua, akilazimika kujifungulia kwenye mkokoteni wa ng'ombe, akipelekwa kituo cha afya Nduruma.

"Ilikuwa mauti na uzima, namshukuru Mungu nilinusurika, lakini ni wanawake wengi wamepoteza maisha katika mazingira kama yangu," anasema.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Fred Kasale, anasema changamoto hizo zingeweza kutatuliwa kwa kujangwa kituo cha afya cha kata ya Bwawani.

**MKONO WA TASAF**

Historia ya kusikitisha inafutwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ambao umejenga kituo cha afya kijijini hapo kitakachohudumia wakazi zaidi ya 20,000 wa Kata ya Bwawani na majirani.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, anasema mradi huo wa afya umebuniwa na wakazi wa Bwawani na kwamba shughuli zote za kijamii zinazofadhiliwa na mfuko huo inaibuliwa na kubuniwa na wananchi.

Anafafanua kuwa majengo manne ya kituo hicho yamegharimu Sh. milioni 600, ambazo zimejenga jengo la wagonjwa wa nje, maabara, wodi ya wazazi, chumba cha kujifungulia na nyumba za watumishi.

Anasema miradi ya TASAF inalenga kuleta mabadiliko kwa vijiji vilivyopo pembezoni, kama ilivyofanyika kijijini Themi ya Simba.

Mziray anafafanua kuwa mradi huo ni sehemu ya ufadhili wa mfuko wa nchi zinazozalisha zaidi mafuta duniani (OPEC), kwa mikoa ya Arusha, Mwanza, Geita, Simiyu na Njombe.

Kwa mujibu wa Mziray, OPEC imetoa Dola za Marekani milioni 50 kufadhili miradi ya kijamii kama afya, elimu na miundombinu katika vijiji vilivyopo pembezoni ambayo itawanufaisha takribani wananchi 900,000.

"Wananchi waliibua mradi huu na TASAF tukaanza kuutekeleza. Tumejenga majengo ya kutolea huduma na nyumba za watumishi, vyote vimegharimu zaidi ya Sh. milioni 600 pamoja na nguvu za wananchi," anaeleza Mziray.

Diwani wa kata hiyo, Justine Siray, anasema Bwanani ilikuwa mbali zaidi na vituo vyote vya afya katika halmashauri hiyo.

"Kutoka hapa hadi Nduruma ni kilometa 10, hapa hadi mjini ni kilometa 50, barabara ni mbaya na usafiri usioeleweka. Wajawazito na wagonjwa walipata shida mno. Ilikuwa tunawabeba kwenye bodaboda, unafika mahali barabara haipitiki mnatafuta ng'ombe, katika kuhangaika huko, mama na mtoto wanapoteza maisha," anasema.

"Hali ilikuwa mbaya kwa wananchi wetu lakini sasa tunaamini itakuwa shwari kwa sababu tutapata huduma hapa nyumbani," anasema Siray.

Anatoa ombi kwa serikali kujenga wodi ya wanaume, wanawake, jengo la utawala, chumba cha kuhifadhi maiti na kichomea taka ili wana Bwani wapate huduma zote sehemu moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Suleiman Msumi, anapokea ombi la wananchi hao na kueleza kuwa kituo hicho kitafunguliwa mwezi ujao kikitazamiwa kuhudumia wanavijiji vya Mungushi, Bwawani, Kigongoni na Themi ya Simba.

"Kitakuwa msaada mkubwa hapa Bwawani na kata jirani hasa kwa wanawake na watoto ambao walikuwa wanapata adha kufuata huduma mbali," anasema.

Msumi anaahidi halmashauri itajenga wodi ya wanaume, wanawake, uzio, tanuru la kuchomea taka na chumba cha maiti; na tayari bajeti ipo.

INAENDELEA UK.12

MAZINGIRA

# Kukausha dagaa juani na mwambani sasa basi, iko nyumba inayotumia jua na gesi

**Na Beatrice Philemon**

JUHUDI za kulinda na kuhifadhi misitu zimeshamiri mojawapo ni ujio wa teknolojia ya kukausha samaki na mazao mengine ya kilimo kwa kutumia nishati ya jua na gesi asili, ijulikanayo kama nyumba ya kukaushia dagaa.

Ni mapinduzi ya kuboresha ukaushaji wa bidhaa unaoanza kutumiwa na wavuvi ndani ya Ziwa Victoria. Teknolojia hiyo, inatarajiwa kufikishwa kwenye visiwa 10 ziwani hapo, hivi sasa inatumiwa kwenye Kisiwa cha Mulumo karibu na Muleba mkoani Kagera, anaeleza Rackson Ngela, mhandisi wa kilimo kutoka kampuni ya Mrutu Agro-Solutions, anapozungumza na Nipashe.

Anasema, teknolojia hiyo itaongeza thamani katika mazao ya baharini kama samaki, dagaa na mazao mengiene ya kilimo yakiwamo mahindi, maharage, mihogo na viazi pia kuinua kipato cha wakulima na wavuvi, huku ikipunguza upotevu wa mazao yao.

Anafafanua kuwa wakati wa msimu wa mvua dagaa wanavuliwa kwa wingi lakini wanapotea kutokana na kukosekana kwa jua la kuwakausha kadhalika na mazao ya kilimo wakati wa msimu wa mavuno ambao hauna jua hupotea pia.

Ngela anazungumzia zaidi dagaa, akisema kuwa kwa muda mrefu, wavuvi wa dagaa ziwani Victoria wamekuwa wakihangaika kupata teknolojia ya kukausha dagaa wakati wa mvua na kuendelea kuwa maskini licha ya juhudi wanazofanya.

Lakini hivi sasa wavuvi kutoka visiwa 10 vilivyopo ndani ya Ziwa Victoria wana kila hali ya kufurahi baada ya Kampuni ya Mrutu Agro-Solutions Company Limited kubuni teknolojia mpya inayotumia mfumo wa ukaushaji wa dagaa au mazao kwa kutumia gesi asilia na joto linalotokana na nishati ya jua kwa ajili ya wavuvi wa dagaa.

Lengo kuu ni kusaidia wavuvi hawa kuinua kipato chao, kupunguza upotevu wa dagaa unaotokana na kuoza au kuharibika, anasema.

"Wakulima wanaitumia pia kukausha mahindi, maharage, mihogo na viazi na wakati wote wa uzalishaji kuanzia kipindi cha mvua, kipupwe na kiangazi." Anasema Ngela.

Mhandisi huyo wa kilimo anasema teknolojia hiyo inapatikana baada ya kufanya utafiti kwa wavuvi wa dagaa wanaoishi katika visiwa 10 vya Ziwa Victoria na kugundua kuwa wakati wa mvua dagaa wanaopatikana kwa wingi wanaharibika kutokana na kukosa teknolojia ya kukausha. Akisema ukaushaji kwenye vichanja katika eneo la wazi uliathiriwa na wadudu na ndege.

"Wakati wa masika kuna dagaa wengi, lakini kuna vipindi vichache vya jua hivyo kupelekea kukaa kwenye vichanja kwa zaidi ya wiki moja na wengi wakaharibika na kutupwa" anasema mhandisi huyo.

Kadhalika aligundua kuwa zaidi ya asilimia 70 ya dagaa wanaovuliwa wanaharibika na kutupwa na biashara ikiwa na changamoto nyingi wakati wa mvua.

Mbali na hilo, kipindi cha kiangazi, dagaa wanapatikana lakini si kwa wingi kama msimu mvua, hata hivyo wakianikwa kwenye vichanja kwa saa 12 hadi 18 wanaliwa na ndege.

Ngele anaongeza kuwa, pia waliona kuna changamoto nyingine ya kupungua ubora wa dagaa kwa sababu wakati zimeanikwa baadhi ya wadudu walitua na kuendelea kukaa kwenye dagaa hadi walipokauka walibakia na kuchafua kitoweo hicho.

"Kutokana na changamoto hiyo tumekuja na mfumo wa kutatua changamoto zote ziwe za kipindi cha mvua, kiangazi, wadudu na ndege ndiyo teknolojia ya 'nyumba ya kukausha dagaa' kwa kutumia joto linalotokana na nishati ya jua na gesi asilia," anasema na kuongeza kuwa nyumba hiyo inaweza kujengwa kwa vyuma au miti na kuta pamoja na paa zake zinafunikwa na nailoni maalumu.

**INAVYOFANYAKAZI**

Mhandisi Ngele, anafafanua kuwa nailoni maalumu zinazozungushwa kwenye nyumba zinasharabu (kunyonya na kuhifadhi) joto la jua na kulihifadhi ndani wakati jua linapokuwa kidogo gesi inajiwasha yenyewe na kuendelea kuzalisha joto katika kuendelea kukausha dagaa, hivyo kufanya joto ndani ya nyumba kuwa kati ya nyuzi joto 50 -70.

Anaongeza kuwa, joto likizidi nyuzi joto 70, gesi inajizima yenyewe na mapanga boi au feni yanawaka na kusambaza joto dagaa waendelea kukauka bila kikwazo.

"Mapangaboi yakizunguka kunakuwa na matundu ya hewa ambayo yanaruhusu hewa iliyofyonza unyevu nyevu kutoka nje," anasema.

**FAIDA YA TEKNOLOJIA**

Mvuvi, atakayetumia teknolojia hii, atapunguza upotevu wa dagaa unaofanywa na ndege, kuoza na wadudu waharibifu, lakini pia uchafuzi unaofanywa na wadudu kwa sababu nyumba hairuhusu wadudu kuingia ndani, anaongeza Ngele.

"Inaongeza ufanisi wa ukaushaji dagaa kutokana na kwamba joto linakuwa limedumishwa kati ya nyuzi joto 50 hadi 70 muda wote huku mvuvi na mfanyabiashara akikausha dagaa wakati wote mchana na usiku, masika, kiangazi au kipupwe kutokana na ufanisi wa teknolojia hii," anaeleza mtaalamu huyo.

Kadhalika, nyumba hii anaweza kukausha bidhaa nyingine endepo mmiliki ataamua na pia anazungumzia eneo, akisema ni dogo lakini linakausha dagaa wengi kwa pamoja.

Anasema nyumba moja yenye ukubwa wa mita 8x 30 ina uwezo wa kukausha tani mbili za dagaa na ni sawa na kuanika katika eneo la wazi lenye zaidi ya ekari moja.

Pia ni rahisi kuzingatia usafi katika nyumba hiyo, hivyo kupata dagaa wanaokuwa na ubora kuliko walioanikwa kwenye miamba, vichanjani na juu ya nyasi.

Ili kusaidia wavuvi, wakulima na wafanyabiashara kuona jinsi teknolojia hiyo inavyofanya kazi, mwaka huu, wanashiriki kwenye maonesho ya Nane Nane- Morogoro ili kuwafikia wateja wao na kutatua changamoto zao kupitia teknolojia za kisasa, anasema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Mrutu Agro-Solutions, Phillipo Mrutu.

Anawakumbusha wavuvi kuwa, baada ya kuvua dagaa, wazichambue, waache zichirizike maji kwa muda wa dakika 10 hadi 15 na baadaye kuwaingiza kwenye nyumba ya kukaushia dagaa, kuna trei ambazo dagaa hupangwa kukauka kwa ufanisi mkubwa wakitumia kati ya saa tano hadi sita kukauka.

Mrutu anasema wakishakauka wanatolewa na kuwekwa mifuko na kuhifadhiwa kwenye ghala ambalo limeijenga karibu na nyumba ya kukaushia dagaa ili kuwatunza kabla ya kupelekwa sokoni.

Anasema wamejenga nyumba ya kukaushia dagaa katika kisiwa cha Mulumo kilichopo ndani ya Ziwa Victoria chenye ukubwa wa mita 30 kwa mita 8 inayokausha tani mbili za dagaa wabichi ndani ya saa tano hadi sita.

Jumla ya wavuvi na wafanyabiashara 24 katika kisiwa hicho wanatarajia kunufaika na teknolojia hiyo, anasema Mrutu na pia wavuvi au wananchi wengine wanaweza kutumia nyumba hiyo kwa makubaliano watakayofanya.

Mbali na hilo, kampuni ina utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wakulima, wavuvi na wafugaji kuhusu teknolojia mbalimbali bora za kilimo, uvuvi na ufugaji.



Nyumba ya kukaushia dagaa inayotumia gesi asilia na jua. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# TASAF ilivyomaliza vilio kuzika kila uchao, ilipojenga hospitali

**INATOKA UK.11**

"Ili kituo cha afya kikamilike kinahitaji majengo saba, hapa yapo manne kwa hiyo yaliyobakia halmashauri tumejipanga kuyakamilisha," anasema.

Msumi anaongeza: "Wananchi tuliibua mradi huu kwa sababu ya umbali wa huduma za afya ambazo wamekuwa wakizifuata zaidi ya kilometa 10 kutoka hapa. Kipindi cha mvua hata kufika Nduruma ni changamoto kubwa, ndio maana tulianzisha mradi huu," anasema.

Anasema kituo kitahudumia zaidi ya wakazi 20,000 wakiwamo wanaotoka Wilaya jirani ya Simanjiro..

"Zahanati tulizonazo hazitoi huduma kama ya upasuaji ambayo tutaipata hapa, kujifungua na maabara ya kisasa. Jengo la OPD hapa lina vyumba vya sindano, vidonda, ofisi za madaktari na duka la dawa," anasema.

Anasema jengo la maabara litafungwa vifaa tiba vya kisasa na vitenganishi kwa ajili ya kutoa vipimo vingi kabla ya matibabu.

"Bwawani iko pembezoni na kufunguliwa kwake kutaleta wataalamu wa afya na kuwapa wananchi huduma nyingine za msingi kama elimu ya afya, chanjo, lishe, usafi na njia za kujikinga na magonjwa hususani ya mlipuko; haya yote yataboresha maisha ya wakazi wa kata hii," anasema na kuongeza kuwa historia sasa imefutwa.

AFYA

# PMI na mkakati kutokomeza malaria

***Mpango wa Rais wa Marekani dhidi ya Malaria (PMI), kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania, unafanya jitihada mbalimbali katika kutokomeza malaria. Mshauri Mkazi na Kiongozi wa Timu ya Malaria, Naomi Serbantez, anabainisha kama alivyohojiwa na MWANDISHI WETU hivi karibuni..***

**SWALI: Unaweza kutueleza nini kuhusu Mpango wa Rais wa Marekani dhidi ya Malaria (PMI), miradi gani inaunga mkono nchini na kwa muda gani imekuwa Tanzania?**

**JIBU:** PMI ni programu ya serikali ya Marekani iliyozinduliwa mwaka 2005 kwa lengo la kupunguza maambukizi na vifo vitokanavyo na malaria katika nchi lengwa. Ni juhudi za pamoja zinazoongozwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID) na kutekelezwa kwa ushirikiano na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC).

Mpango huu unalenga nchi zenye maambukizi makubwa ya malaria hasa zilizoko Africa, Asia na Amerika ya Kusini. Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi tatu za kwanza kupokea ufadhili chini ya PMI mwaka 2006. Hadi sasa, Tanzania imepokea zaidi ya DOla milioni 747 kusaidia mapambano dhidi ya malaria Tanzania Bara na Zanzibar.

Lengo kuu la PMI ni kuunga mkono juhudi za Tanzania kudhibiti na kuondoa malaria kupitia usambazaji wa vyandarua vyenye dawa, upuliziaji wa dawa za kuua mbu ndani ya nyumba, matibabu ya kuzuia malaria kwa wajawazito, na uchunguzi wa haraka na matibabu.

PMI pia inalenga kuboresha uwezo wa wafanyakazi wa afya, kuimarisha usimamizi wa ugavi wa bidhaa za malaria, kusaidia mifumo ya ufuatiliaji na mawasiliano yenye lengo la kubadili tabia za watu katika kupambana na kujikinga na malaria.

**SWALI: Wewe ni Mwanamke wa kwanza Mtanzania kuteuliwa Mshauri Mkazi wa PMI na Kiongozi wa Timu ya Malaria katika USAID/Tanzania. Uteuzi huu una maana gani kwako na Tanzania inafaidika vipi na nafasi yako?**

**JIBU:** Uteuzi huu ni hatua muhimu kwangu na kwa taaluma ya afya ya umma. Hii ni kutambua ujuzi wangu, kujitolea kwangu na michango yangu katika kudhibiti malaria na afya ya umma. Pia inathibitisha juhudi kubwa na kujitolea nilizowekeza katika kupambana na malaria na kuboresha afya Tanzania.

Hii pia ni fahari kubwa kwangu na natumaini mafanikio yangu yatatia moyo Watanzania wengine, hasa vijana, kufuata taaluma katika afya ya umma. Nafasi hii inakuja na jukumu kubwa la kuongoza juhudi za kudhibiti malaria na inatoa fursa ya kuleta maarifa na mitazamo ya ndani kwenye mikakati ya PMI kwa muktadha wa Tanzania.

Uteuzi wangu unaonyesha kutambulika kwa uwezo wa wataalamu wa afya wa ndani ya nchi. Inaangazia umuhimu wa kuhusisha ujuzi wa ndani katika nafasi za uongozi ili kushughulikia changamoto za afya kwa ufanisi zaidi.

Kuwa na Mtanzania katika nafasi hii, kunaimarisha ushirikiano kati ya wadau wa ndani na wa kimataifa, kudumisha ushirikiano, kuhakikisha ulinganifu na vipaumbele vya kitaifa, na kukuza njia jumuishi za kudhibiti malaria na mipango ya afya ya umma.

Nikiwa mwanamke katika uongozi, uteuzi huu unaongeza utofauti wa uongozi katika mipango ya afya ya kimataifa na kuonesha umuhimu wa uwakilishi na ujumuishi katika kushughulikia changamoto za afya ya kimataifa. Pia inaonesha kutambuliwa kimataifa kwa maendeleo katika afya ya umma Tanzania na kuvutia rasilimali kusaidia mipango ya afya kwa sasa na siku zijazo.

**SWALI: Ukiwa Mshauri Mkazi wa PMI na Kiongozi wa Timu katika kuongoza mpango wa pili kwa ukubwa wa PMI duniani wa programu ya dola milioni 44 kwa mwaka, fedha hizi zinatumikaje katika kupambana na malaria Tanzania?**

**JIBU:** Kusimamia mpango mkubwa wenye bajeti ya Dola milioni 44 kwa mwaka, ni muhimu sana kutenga fedha hizi kimkakati ili kuongeza mafanikio katika kudhibiti na kuondoa malaria. Kwa kutenga fedha kimkakati katika hatua zilizothibitishwa na WHO, mpango wa PMI unalenga kupunguza maambukizi, kupunguza maradhi na vifo vitokanavyo na malaria hatimaye kufikia lengo la kuondoa malaria nchini.

**SWALI: Je, ni miradi gani muhimu ya malaria ambayo PMI inaipa kipaumbele nchini kwa sasa?**

**JIBU:** Kama nilivyotaja hapo awali, kwa Tanzania (Bara na Zanzibar), PMI inazingatia hatua kadhaa za mapambano ili kuondoa kabisa malaria. Maeneo muhimu ya kipaumbele ni:

Kwanza, udhibiti wa mbu. PMI inasaidia ununuzi na usambazaji wa vyandarua vyenye dawa za kuua mbu kwa kaya, shule za msingi na vituo vya kutolea huduma za afya kupitia kliniki za uzazi na chanjo.

Pili, uchunguzi na matibabu ili kuimarisha uwezo wa uchunguzi wa malaria kwa kutoa vipimo vya haraka (RDT) na kuboresha huduma za maabara kuhakikisha uchunguzi wa malaria kwa usahihi na kwa wakati. Pia kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa dawa za malaria, hasa dawa mseto (ACT).

Tatu, malaria kwa wajawazito kuhakikisha wajawazito wanapata matibabu ya kuzuia malaria wakati wa kliniki za uzazi ili kuwalinda wao na watoto ambao hawajazaliwa.

**SWALI: Kiwango cha maambukizi ya malaria Tanzania kilishuka kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia saba mwaka 2022. Je, ushirikiano na PMI umeisaidiaje kufikia hatua hii?**

**JIBU:** Hali hii ilichangiwa na juhudi za pamoja kati ya serikali ya Tanzania, PMI, Mfuko wa Dunia na wadau mbalimbali wa malaria. PMI inakamilisha juhudi za serikali ya Tanzania kwa kusaidia Mipango ya Kitaifa ya Mkakati wa Malaria.

**SWALI: Licha ya juhudi, rasilimali na utaalamu kuwekezwa katika kuondoa malaria Tanzania, ugonjwa huu bado uko juu na unaua mamilioni ya watoto na wajawazito. Tanzania inakosea wapi licha ya juhudi hizi zote?**

**JIBU:** Ni kweli pamoja na juhudi zote na mafanikio ambayo Tanzania imeyapata, bado malaria inabakia na changamoto kubwa ya kiafya hasa kwa watoto wadogo na wajawazito. Kuna mambo mengi yanayozuia maendeleo kuelekea kutokomeza malaria kama vile upatikanaji na matumizi ya vyandarua vyenye dawa. Pale ambapo vyandarua vinapatikana, baadhi ya kaya hazitumii ipasavyo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mila potofu.

Sababu nyingine ni tabia ya wananchi kuchelewa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya waonapo dalili za malaria kama homa. Hali hii pia inachangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo vikwazo vya kifedha kusababisha kuchelewa kupata huduma za afya na kufanya mgonjwa kuzidiwa na kifo.

Nyingine, usugu dhidi ya viuatilifu na dawa zinazotumika kutibu wa malaria, mnyororo wa ugavi pia unaweza kusababisha upungufu wa bidhaa muhimu kama vyandarua, vipimo vya haraka (RDT) na dawa. Uwezo mdogo wa wafanyakazi wa afya, ukosefu wa motisha, na mgawanyo wa wafanyakazi wa afya, vinaweza kupunguza ufanisi.

Vitu vya mazingira kama nyumba duni, hali ya maisha, mabadiliko ya hali ya hewa, na vitendo vya kilimo vinaweza kusababisha kuzaliana kwa mbu na usambazaji wa malaria. Ushirikishwaji hafifu wa jamii na umiliki wa juhudi za kudhibiti malaria kunaweza kusababisha ushiriki mdogo katika hatua za kuzuia.

PMI, serikali na wadau wengine wa malaria wanashughulikia changamoto hizi kwa kuimarisha mifumo ya usambazaji, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, kupambana na upinzani, kuboresha usimamizi wa mnyororo wa ugavi, kufundisha na kusaidia wafanyakazi wa afya na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji pamoja na kushirikisha jamii.

INAENDELEA UK.14



Mshauri Mkazi na Kiongozi wa Timu ya Malaria, Naomi Serbantez.

> Kama nilivyotaja hapo awali, kwa Tanzania (Bara na Zanzibar), PMI inazingatia hatua kadhaa za mapambano ili kuondoa kabisa malaria.

AFYA

# Baba pombe unazokunywa

• Ni chanzo cha mimba dhaifu, watoto wenye kasoro na maradhi sugu

Na Moshi Lusonzo

ZAIDI ya miaka 50, wanasayansi wameonya kuhusu hatari za kunywa pombe kupita kiasi kwa wajawazito.

Safari hii utafiti unabaini kuwa mwanaume kunywa kupindukia pia kunaathiri kutunga na ukuaji wa mtoto. Utafiti huo unagundua kuwa, unywaji wa pombe hata mara moja kwa wiki, unaweza kuathiri ukuaji wa ubongo wa mtoto aliye tumboni, ufahamu, tabia na taswira ya uso.

Kuna madhara ya kuharibika kwa mfumo wa mishipa ya fahamu, mtoto kuwa na uwezo mdogo wa kujifunza na kuchelewa kuongea. Wataalamu wanasema hakuna kiwango salama cha pombe anachotakiwa kunywa mwanamke mjamzito.

Imefahamika kuwa, hatari za kunywa pombe kwa mama ndizo zinaelezwa kumwathiri mtoto tumboni, lakini athari zinazotokana na unywaji pombe kwa baba zinapuuzwa.



### BABA MBAYA ZAIDI

"Kwa miaka sasa, tumekuwa tukisikia hadithi kutoka kwa wanawake wakisema hawakuwahi kunywa pombe wakati wa ujauzito, lakini wamepata watoto wenye matatizo."

Wanajieleza zaidi kuwa waume zao au wenza walikuwa wanywa pombe kwa muda mrefu, anasema Michael Golding, ambaye ni mwanafiziolojia katika Chuo Kikuu cha Texas, A&M Marekani.

Golding amejikita katika utafiti wa madhara ya pombe kwa wajawazito.

Anasema utafiti umebainisha kuwa, kutumia pombe kwa kinababa kunahusishwa na matatizo mbalimbali ya ukuaji na ukomavu wa akili kwa watoto na wako katika hatari kubwa ya kupata matatizo ya kiafya.

Utafiti wa 2021, uliochunguza zaidi ya wanandoa 500,000 nchini China, uligundua hata kama mama sio wanywaji wa pombe walikuwa hatarini kupata watoto wenye matatizo.

Walizaliwa na mdomo uliopasuka, magonjwa wa moyo na matatizo kwenye tumbo, yote hayo yakisababishwa na baba aliyekunywa pombe wakati wa kutungwa kwa mimba.

Utafiti mwingine kutoka China uliwachunguza watoto 5,000 wenye matatizo ya moyo na 5,000 wasio na matatizo, iligundulika kuwa walikuwa hatarini mara tatu zaidi ya kuwa na matatizo ya moyo ya kuzaliwa ikiwa baba ni mnywaji katika kipindi cha miezi mitatu kabla ya ujauzito, kuliko baba asiyetumia pombe.

"Utafiti wetu unapendekeza kwamba kina baba wanapaswa kurekebisha unywaji wa pombe kabla ya mama kushika ujauzito ili kupunguza hatari ya mtoto kuzaliwa na matatizo," anasema mtafiti Golding.

Anaongeza: "Kwa kuzingatia kwamba kiwango cha unywaji wa baba cha asilimia 31.0 huongeza hatari ya mtoto kuzaliwa na kasoro."

Watoto wenye matatizo yaliyotokana na mzazi kunywa pombe hulazwa mara nyingi hospitalini kuliko wale wasiokuwa na wazazi walevi.

Kutumia pombe kwa wanaume kunatahadharishwa kuwa, kadiri anavyokunywa ndivyo anavyoongeza hatari kwa mtoto na matokeo yanavyozidi kuwa mabaya.

Kama ilivyo kwa sigara, kuna uthibitisho kuwa kuvuta sigara kunaathiri chembe za urithi au nasaba (DNA).

Watoto wanaozaliwa na baba wanaovuta sigara wana uwezekano mkubwa wa kuwa na kasoro za kuzaliwa, kupata saratani ya damu na kuwa na mafuta mengi mwilini.

### BADILI MTIZAMO

Licha ya kunywa pombe kwa wanaume kunaonekana pia kuathiri watoto, watafiti wengi wanakubali kuwa pombe kwa mama huathiri zaidi katika ukuaji wa mtoto.

Hiyo inatokana na damu yake kupitishwa moja kwa moja hadi kwa mtoto kupitia kondo (plasenta) kwa hivyo, ni athari ya moja kwa moja katika ukuaji.

### ATHARI ZAIDI

Daktari na profesa wa afya ya watoto na vijana katika Chuo Kikuu cha Sydney nchini Australia, Elizabeth Elliott, ametafiti kwa muda mrefu athari za pombe kwa mimba changa akisema kilevi huathiri ubongo wa mtoto.

"Pombe inaathiri ubongo na sehemu ya ubongo ambayo huamua muonekano wa uso na inaathiri maendeleo ya mifumo yote ya viungo kama mapafu, moyo, masikio na macho," anasema Elliott.

Elliott na wengine wanasema wakati umefika kuwa na kampeni za afya kwa umma itakayokataza kunywa pombe kwa kina baba moja kwa moja.

"Hatuna data kamili, kuna mambo mengi ambayo tunajua yanaweza kuboresha afya kwa watoto, kama vile kufanya mazoezi na kula vizuri. Kama wangekuwa wanangu, ningewaambia waache pombe," anaongeza.

Anasisitiza, "kuna mzigo mkubwa ambao hutwishwa wanawake, lakini afya ya mwanaume ni muhimu kwa ukuaji wa mtoto tumboni na hili ni jukumu la pande zote mbili hapa kusaidia na kutoa afya ya mtoto."

# PMI na mkakati kutokomeza malaria

INATOKA UK.13

**SWALI: Zanzibar ilikumbwa na ongezeko la malaria licha ya mafanikio ya zamani kutokana na mabadiliko ya tabianchi. PMI inakabiliana vipi na changamoto hii kuhakikisha haijirudii tena?**

**JIBU:** PMI kwa kushirikiana na Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP) na wadau wengine wa malaria chini ya Wizara ya Afya Zanzibar, inashughulikia changamoto ya ongezeko la malaria kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Mikakati muhimu ni pamoja na:

Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na mapambano ya haraka: Mkakati ni Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa malaria ili kugundua na kupambana na malaria kwa wakati, ikijumuisha ukusanyaji wa taarifa kwa wakati na uchambuzi wa kufuatilia mwenendo wa malaria na kutambua milipuko mapema.

Usimamizi jumuishi wa dawa za kuua mbu kwa kusambaza vyandarua vyenye dawa na kufanya kampeni za upuliziaji wa dawa ndani ya kuta za nyumba.

Kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi: Kuendeleza na kutekeleza mikakati ya kudhibiti malaria inayostahimili mabadiliko ya tabianchi kama vile kutumia mbinu za usimamizi wa mazingira, kupunguza maeneo ya kuzaliana kwa mbu na kuondoa maji yaliyotuama.

Kuboresha Uchunguzi na Matibabu kwa kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya vifaa vya kupima malaria katika vituo vya afya pamoja na upatikanaji wa dawa za kutibu malaria kwa ufanisi. Kuhakikisha wafanyakazi wa afya wamefundishwa ipasavyo kupima na kutibu malaria.

Ushirikishwaji wa Jamii na Elimu: Kutekeleza kampeni za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia ili kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulala ndani ya chandarua chenye dawa kila siku, kwenda kituo cha kutolea huduma za afya uonapo dalili yoyote ya malaria hasa homa na kuzuia malaria Pamoja na ushirikishaji wananchi.

Kuimarisha Mifumo ya Afya: Kufanya kazi kwa karibu na serikali ya Tanzania, mamlaka za afya za ndani, mashirika yasiyo ya kiserikali, na wadau wengine ili kuhakikisha juhudi za pamoja na za kina za kudhibiti malaria.

**SWALI: Inatabiriwa kwamba Tanzania itaweza kutokomeza malaria ifikapo mwaka 2050. Kwa sasa Tanzania bado ni moja ya nchi 11 duniani yenye maambukizi na vifo vya malaria. Kuna umbali kiasi gani kufikia lengo hili?**

**JIBU:** Tanzania imepiga hatua nzuri katika kupunguza maambukizi ya malaria, lakini kufikia kutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2050 kunahitaji juhudi zaidi, ubunifu, na ushirikiano wa kudumu kati ya serikali, mashirika ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii. Malengo ni makubwa lakini yanatekelezeka kupitia kujitoa na kutekeleza mikakati iliyowekwa.

**SWALI: Rais mstaafu Jakaya Kikwete alishauri Baraza la Kutokomeza Malaria Tanzania kuongeza juhudi kwa kutumia mikakati iliyofanikiwa kutokana na changamoto zilizopo. Je, nini mtazamo wako?**

**JIBU:** Kudhibiti malaria Tanzania kunahusisha juhudi za pamoja za kuongeza mikakati iliyofanikiwa na kukabiliana na changamoto zinazoibuka. Pia uwapo wa utashi wa kisiasa, ufadhili endelevu na ushirikishwaji wa sekta binafsi na jamii, Tanzania inaweza kufanya maendeleo zaidi katika kupunguza mzigo wa malaria.



# Mvinyo utokanao na asali wabuniwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ILI kuongeza thamani ya zao la asali nchini, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimekuja na ubunifu wa kuzalisha mvinyo utokanao na zao hilo.

Mkurugenzi Mawasiliano na Masoko UDOM, Rose Joseph, alibainisha hayo jana kwenye maonesho ya wakulima kitaifa yanayofanyika viwanja vya Nzuguni jijini hapa.

Alisema pamoja na mambo mengine chuo hicho kimekuwa kikijihusisha na ufugaji nyuki na kuzalisha zao la asali na mazao mengine yatokanayo na nyuki.

"Chuo Kikuu cha UDOM, katika maonesho haya kimekuja na ubunifu wa kutumia zao la asali kuzalisha mvinyo ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na nyuki nchini" alisema.

Alisema mazao mengine wanayozalisha yatokanayo na nyuki ni pamoja asali na nta.

Rose alisema pia UDOM, wamebuni teknolojia ya rahisi ya ufugaji samaki ambayo wananchi wanaweza kuitumia kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi.

Alisema: "Katika teknolojia hii tumebuni mfumo ambao unaweza kuutumia kulisha chakula samaki hata kama hautakuwepo eneo husika kwa kuseti muda na chakula kiasi gani unataka walishwe".

**"Chuo Kikuu cha UDOM, katika maonesho haya kimekuja na ubunifu wa kutumia zao la asali kuzalisha mvinyo ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na nyuki nchini"**

Aidha, alisema ubunifu mwingine ni teknoloji ya kubaini magonjwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiwakabili wafugaji na kupunguza tija ya mifugo nchini.

"Ubunifu mwingine ni ufugaji wa sungura kisasa ambapo mkojo wake unatumika kama viuatirifu kwenye mimea ya bustani lakini kinyesi chao kinatumika kama mbolea hivyo kuondoa matumizi ya kemikali" alisema.

Kadhalika, alitoa wito kwa vijana wenye sifa kujiunga na kozi mbalimbali ambazo zinatolewa na chuo hicho hivi sasa.

Alisema: "Dirisha la usajili lilishafunguliwa tangu Julai hivyo niwaombe watu wenye sifa kuomba kujiunga na chuo chetu ili wapate ujuzi utakaowasaidi kujiajiri na kuwa chachu katika jamii zao".



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Afya, Dk. Festo Dugange (kulia), akizungumza jambo na maofisa wa Ofisi ya Makamu wa Rais, alipotembelea banda la ofisi hiyo katika Maonesho ya Kilimo Nanenane, kwenye Viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma juzi. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara waitwa kujenga vituo vya mafuta vijijini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imewahamasisha wafanyabiashara wa mafuta kuwekeza vituo vya bidhaa hiyo maeneo ya vijijini ili kukomesha tabia ya uuzaji holela kwenye vidumu.

Mkaguzi wa mafuta, EWURA Kanda ya Kati, Arthur Lyatuu, alisema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya wakulima kitaifa yanayofanyika viwanja vya Nzuguni jijini hapa.

"Tunajitahidi kuhamasisha watu wajenge huduma hii kule vijijini kwasababu huduma hizi za vituo vya mafuta siyo vingi kwani watu wanakimbilia mijini kutokana na sababu mbalimbali.

"Wengine wanakimbilia mjini kwasababu ya ulinzi na miundombinu ya benki na barabara, vijiji wanakwenda lakini siyo sana, wajitahidi kuweka vituo ili kuondoa hatari iliyopo sasa ya watu kufanya biashara hiyo kwa kificho na hatarishi"alisema.

Aidha, alisema hivi sasa maeneo ya vijijini kunahatari kubwa, kwamba watu wanafanya biashara ya mafuta kwa njia ya kificho ikiwemo kuuza kwenye vidumu.

"Hiyo tabia tunaipiga vita tukikamata mtu anakiasi kikubwa cha mafuta tunamshauri afungue kituo kidogo ili afanye biashara hiyo kwa njia salama kuliko kuweka kwenye madumu makubwa ambayo yanaweza kuleta mlipuko kwenye makazi ya watu" alisema.

Lyatuu alisema mafuta yanapokuwa kwenye matangi ya chini ya ardhi siyo rahisi kulipuka kwakuwa yanakuwa salama sana.

Kadhalika, alisema ili kuhamasisha uwekezaji wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini, EWURA ililegeza masharti ikiwemo kupunguza gharama za maombi.

"Mtu ambaye anataka kuwekeza kituo cha mafuta kijiji mamlaka ililegeza masharti ambapo ukituma maombi ya kutaka kujenga unalipa Sh. 50,000 lakini mjini unalipa Sh. 500,000 wakati hapo awali hali ilikuwa gharama sawa kwa maeneo yote" alisema.

Vile vile, alisema masharti ya ukaguzi wa eneo la ujenzi wa kituo cha mafuta kijijini ni tofauti na ilivyo mjini.

Alisema: "Mjini lazima ukaguliwe na Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) lakini kijiji ukaguzi unaweza kufanywa na halmashauri husika na mwombaji kuandikiwa barua na Mkurugenzi wa Halmashauri na kuanza ujenzi".

# Wakulima watakiwa kuacha kilimo cha kuhama

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

OFISA Mazingira Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Innocent Makomba, amewataka wakulima kuacha kilimo cha kuhama.

Amesema aina hiyo ya kilimo kimekuwa kikisababisha uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti ovyo.

Alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya wakulima kitaifa katika viwanja vya Nzunguni jijini hapa. Makomba alisema kilimo hicho cha kuhamahama kimekuwa kinasababisha ukataji miti ovyo na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Alisema kilimo hicho pia kimekuwa kikisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira hali ambayo imekuwa ikichangia kutokupata mvua za kutosha na kwa wakati na uwepo wa jangwa kutokana na kukosekana kwa uoto wa asili.

Hivyo, aliwataka wakulima kwenye maonyesho ya kilimo kutumia fursa ya teknolojia zinazotolewa za kisasa kwa malengo ya kujiongezea elimu na kipato kupitia sekta hiyo pamoja na ufugaji.

Alisema: "Tekolojia hiyo ikifanyika katika sekta hizo za kilimo, ufungaji na biashara zitaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira kwa kuwa wafugaji wataepuka kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji na wakulima wataepukana kulima kwenye vyanzo hivyo vya maji".

Kadhalika, alisema NEMC itaendelea kutoa elimu kwa sekta zote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa kupitia uratibu, uwezeshaji, elimu ya usimamizi wa sheria na kufuatilia utafiti wa mazingira.

Alisema: "Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira majukumu mengine yaliyopo ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kusaidia taasisi na asasi mbalimbali zinazohusika na usimamizi wa maliasili na mazingira".

Alisema usimamizi huo ni pamoja na uhamasishaji wa ujengaji wa majosho ya kuongesha na kunyweshea mifugo ili wasiharibu vyanzo vya maji.

# Polisi wapigwa msasa kuelekea Uchaguzi S/Mtaa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

ASKARI wa Jeshi la Polisi wametakiwa kutambua wajibu wao wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tangu kuanza kwa mchakato, kampeni, kupiga kura, wakati wa kutangaza matokeo na kuapishwa kwa viongozi watakaochaguliwa.

Mjumbe wa Dawati la Uchaguzi Taifa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Lupisio Mwakyusa, kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai Nchini alisema hayo juzi alipokuwa akitoa elimu ya uchaguzi kwa maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali wilayani Manyoni mkoani Singida.

Mwakyusa alisema kuwa wajibu wa polisi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni pamoja na kulinda mikutano ya kampeni, wagombea, viongozi wa serikali kutoka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, vifaa vya kupigia kura, wapiga kura na miundombinu mingine ya uchaguzi.

Alisema askari wanatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi ili iwe rahisi kwao kuzitekeleza, hivyo uchaguzi kufanyika kwa amani na utulivu. Aidha, aliwataka wananchi wenye sifa za kupigiwa au kupiga kura kujiandaa kuchagua au kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi huo ili kupata viongozi wanaofaa.

Alisema: "Kila mwananchi mwenye sifa ya kupiga au kupigiwa kura anao wajibu wa kuzifahamu na kuzifuata sheria, taratibu na miiko ya uchaguzi tangu kuanza kwa mchakato hadi kuapishwa kwa washindi katika uchaguzi huo".

Naye Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Elisante Olomy kutoka Kitengo cha Polisi Jamii, aliwataka wanachi wanaotarajia kugombea kutojiingiza katika imani za kishirikina kwa kuamini kuwa watashinda uchaguzi.



# Wawili mbaroni kwa kukutwa na bunduki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na bunduki bila kuwa na kibali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Benjamin Kuzaga, alitoa taarifa hiyo juzi mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa katika basi la abiria wakisafiri.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Sebastian Thomas (37) ambaye ni dereva na mkazi wa Isanga na Silvester Mashauri (40) mkazi wa Iganzo jijini Mbeya.

Kamanda Kuzaga alisema bunduki waliyokamatwa nayo watuhumiwa hao ni yenye namba za usajili C328809 na kwamba watu hao walikuwa hawana nyaraka ya aina yoyote inayoonesha uhalali wa kuimiliki silaha hiyo.

Alisema mtuhumiwa Sebastian alikamatwa akiwa na silaha hiyo akiwa ameificha kwenye mfuko wa sandarusi na kuiweka nyuma ya kiti cha dereva ndani ya gari lenye namba za usajili T. 844 DME aina ya Tata inayosafirisha abiria kati ya jiji la Mbeya na Chunya.

Alisema mtuhumiwa baada ya kukamatwa alieleza kupewa silaha hiyo na mwenzake Silvester kwa ajili ya kwenda kutumika katika shughuli za ulinzi machimboni katika kampuni binafsi wilayani Chunya.

**"Alisema alikuwa anakwenda kuipeleka kwenye machimbo ya dhahabu wilayani Chunya jambo ambalo haliruhusiwi kwa mujibu wa sheria za umiliki wa silaha"**

"Alisema alikuwa anakwenda kuipeleka kwenye machimbo ya dhahabu wilayani Chunya jambo ambalo haliruhusiwi kwa mujibu wa sheria za umiliki wa silaha kuazimana kwa mtindo huu, kwa hiyo tunaendelea kuwashikilia kwa ajili ya mahojiano," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema kwa mujibu wa sheria kila mtu anayemiliki silaha za moto ni lazima awe na kibali maalumu ambacho kinamruhusu kumiliki na kwamba yeyote anayekutwa anamiliki bila kibali atachukuliwa hatua za kisheria.

Katika hatua nyingine Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo linamshikilia kijana mmoja aitwaye Lugano Tutufye (29) mkazi wa RRM Ilomba jijini Mbeya kwa tuhuma ya kupatikana na silaha ya wizi.

Alisema kijana huyo alikamatwa na silaha (bastola) aina ya Browing ikiwa na risasi tisa ndani ya magazine mali ya Said Mwatuka (46) mkazi wa Chamazi jijini Dar es Salaam.

Alisema awali Agosti 04 mwaka huu katika moja ya hoteli zilizopo eneo la Nanenane jijini Mbeya, Mwatuka aliibiwa silaha hiyo iliyokuwa ndani ya gari lake aina ya Subaru lenye namba za usajili T.410 DYB.

Alisema mtuhumiwa wa wizi wa silaha hiyo alipakiwa na mmiliki wa silaha hiyo kwenye gari kama abiria na ndipo akafanikiwa kuichukua na kutokomea nayo.



Wadau wa Kilimo Ikolojia, Maria Mathias (kushoto) na Austino Thomas wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia mbegu bora za kisasa za mahindi na maboga kwa mkulima kutoka wilayani Kilosa, Tatu Maganga, alipotembelea maonesho ya kilimo ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Nzunguni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC: Wakulima wapewe elimu bima ya mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeishauri Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo ya vijijini kuhusu umuhimu wa bima katika kulinda afya zao na mali wanazomiliki yakiwamo mazao ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa ushauri huo juzi wakati wa ziara ya Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware na baadhi ya watendaji wa mamlaka hiyo mkoani Mbeya.

Viongozi hao walifanya ziara hiyo ikiwa ni mwendelezo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, yenye lengo la kuwahamasisha wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuhusu utekelezaji wa sheria ya bima na kutambulisha ofisi ya kanda.

Homera alisema mikoa ya kanda hiyo ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na hivyo wananchi wanahitaji kupatiwa elimu kuhusu bima ili wakate kwa ajili ya kuyalinda mazao hayo. Alisema endapo wananchi watahamasishwa na kukata bima itakuwa rahisi kufidiwa na kampuni za bima endapo yatatokea matatizo yoyote kwenye mazao yao.

Vilevile, alisema elimu kuhusu bima ya afya kwa wote ni muhimu ikaendelea kutolewa kwa wananchi wa maeneo yote nchini, ili utekelezaji utakapoanza wananchi wawe na uelewa wa kutosha.

Kamishna wa Bima, Dk. Saqware alisema mamlaka hiyo inaendelea na maandalizi ya mpango maalumu wa miaka mitano wa kutoa elimu kwa wananchi ambao unatarajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2025 mpaka 2030.

Alisema kabla ya kuanza kutekeleza mpango huo waliamua kukutana na wakuu wa mikoa na kuwahamasisha kuhusu usimamizi wa sheria ya bima ili na wao washiriki kwenye hamasa hizo.

Alisema mbali na wakuu wa mikoa pia wanakutana na wakuu wa wilaya pamoja na makundi ya baadhi ya vijana hasa waendesha pikipiki ili na wao wajue umuhimu wa kukata bima vyombo vyao.

Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti na Maendeleo ya Masoko ya Bima, Samwel Mwiru alisema sekta ya bima kwa sasa inaendelea vizuri nchini kwa maelezo kuwa inakua kwa asilimia 15 kila mwaka, huku ikichangia asilimia mbili kwenye pato la taifa.

Alisema wananchi wameanza kuwa na mwamko mzuri wa kukata bima ikilinganishwa na miaka ya nyuma, huku akieleza kuwa zaidi ya asilimia 95 ya madai ya bima huwa yanalipwa kwa wakati kupitia mikataba mbaimbali.

Meneja wa TIRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Neema Mtuha, alisema kanda hiyo inahudumia mikoa mitatu ambayo ni Mbeya, Songwe na Njombe.

Alisema wamekuwa wakitembelea maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo kila mwaka kulingana na bajeti kwa lengo la kuhamasisha wananchi kujiunga na bima pamoja na kufuatilia malalamiko ya wateja wa bima na kuyatatua.

## Wananchi kicheko serikali ikiwajengea barabara

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WANANCHI kutoka vijiji sita vya kata za Mawengi na Makonde Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, wameishukuru serikali kwa kujenga Barabara ya Mawengi-Kimata hadi Makonde (Km 28) wakidai itasaidia usafiri na usafirishaji.

Wakizungumza na Nipashe wananchi hao walisema kwa muda mrefu wamekuwa wakisafiri ziwani kwa kutumia mitumbwi au kutembea zaidi ya kilomita 30 kutoka kata hiyo hadi kata za jirani kwa ajili ya kupata mahitaji mbalimbali na huduma za kijamii zikiwamo afya.

Mmoja wa wananchi hao, Joshua Haule alisema kwa miaka mingi wamekabiliwa na tatizo la kubeba mazao kichwani kwenda kuuza vijiji jirani ili kupata fedha ya kusomesha watoto wao.

"Tunasomesha watoto kwa kubeba mizigo kichwani ni shida sana lakini hivi sasa imeisha, tutasafirisha mazao yetu kwa magari," alisema Haule.

Victoria Mwinuka alisema tatizo lao kubwa lilikuwa ni kukosekana kwa barabara ambayo ilikuwa ikisababisha wajawazito kujifungulia njiani au vifo kwa sababu ya kushindwa kufika hospitali.

Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Ludewa, Butene Jilala alisema barabara hiyo inapita Mawengi-Kimata- na Makonde (Km 28) kwa Sh. bilioni 1.436 na inatarajia kunufaisha wananchi 5,220.

Jilala alisema kazi zilizofanyika ni pamoja na kukata na kulipua milima kwa lengo la kufungua barabara, kujenga zege, kujenga madaraja madogo na kuchonga barabara.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Victoria Mwanziva, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa sababu inakwenda kupandisha uchumi na maendeleo kwa wananchi hao.

Alisema: "Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu wa barabara. Barabara ni maendeleo, barabara ni uchumi kwa hiyo tunaishukuru serikari kwa kutushushia Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya kuchonga barabara".

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema barabara hiyo imejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni mbili za maombi maalumu ambazo ni nje ya bajeti na hivyo kutumika kujenga barabara ya Lifuma na Makonde.

Kamonga alisema wananchi hao wameteseka kwa miaka mingi tangu uhuru kwa sababu magari kushindwa kufika kutokana na kukosa barabara, kwamba ilisababisha kushindwa kusafiri pamoja na kusafirisha mazao yao kwenda vijiji vya jirani.

## Chuo Kikuu Fudan, ZAHRI kushirikiana katika utafiti

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu cha Fudan kutoka Shanghai China kimeahidi kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) katika utafiti, ambazo zitasaidia kuleta mageuzi katika masuala ya afya ya binadamu.

Hayo yalisemwa na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Zhenghong Yuan, alipofanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI), Dk. Mayasa Salum Ali.

Prof. Yuan alisema Chuo Kikuu cha Fudan kinauzoefu mkubwa katika masuala ya kufanya kazi za utafiti zinazohusiana na masuala ya binadamu, kwamba kina hospitali 14 zinazotoa huduma za matibabu.

Hivyo, aliahidi kuendeleza makubaliano ya ushirikiano yaliyofikiwa ambayo ni MOU iliyotiwa saini mwaka jana nchini China katika kubadilisha wataalamu pamoja na kutoa nafasi za elimu ya juu.

"Tunayo makubaliano ya mashirikiano ya MOU ambayo yamefikiwa na pande mbili ambapo tunaahidi kutekelezwa na kusimamiwa kwa maslahi ya pande mbili katika masuala muhimu ya utafiti yanayohusisha masuala mbali mbali ya afya ya binaadamu"alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti na Afya, Dk. Mayasa Salum Ali alisema ujio huo umelenga kuendeleza ushirikiano ya pande mbili katika masuala ya kazi za utafiti zinazohusisha maeneo mbalimbali ikiwemo afya ya binaadamu.

Dk.Mayasa aliyataja mahitaji makubwa ya Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar ni wafanyakazi wake kupata viwango vya elimu ya juu katika masuala mbalimbali hatua ambayo itawawezesha kufanya kazi za kitaalamu.

Mratibu wa Uhusiano katika Chuo Kikuu cha Fudan, Prof. Yiayan Huang, alisema lengo la ziara hiyo ni kubadilisha mawazo kuona mambo mbali mbali ikiwamo mahitaji kwa upande wa Taasisi ya Utafiti ya Afya Zanzibar.

Alisema wamejifunza mengi katika ziara yao juu ya ushirikiano kwa upande wa Zanzibar katika kukuza nyanja ya kazi za utafiti.

Ujumbe huo ulipata nafasi ya kutembelea Hospitali ya Mnazi Mmoja na kuonana na wataalamu na madaktari kutoka China wanaofanya kazi Zanzibar pamoja na kutembelea Hospitali ya Mkoa iliopo Lumumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

# Serikali kuboresha miundombinu maeneo ya viwanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inadhamira ya kuhakikisha kuwa maeneo yaliotengwa kwa ajili ya viwanda yanawekewa miundombinu muhimu, ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi eneo la mradi wa kimkakati wa uwekezaji wa viwanda Dunga Zuze Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema hatua hiyo pia inalengo la kuchochea masuala ya kiuchumi katika nchi, kuimarisha na kuyaendeleza maeneo ya viwanda ni sehemu ya kuondoa mpango wa umaskini na kuongeza kipato kwa wananchi kupitia ajira.

Alisema uwekaji huo wa msingi ni mpango wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050, Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 na Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar ambao umelenga kukuza mchango wa sekta ya viwanda kwenye uchumi kutoka asilimia 19 mwaka 2029 hadi asilimia 35 ifikapo mwaka 2050.

Aidha, alisema mradi huo utatoa faida mbalimbali ikiwamo fursa za ajira kwa vijana, uingizaji wa thamani wa mazao ya wakulima na wafugaji pamoja na kuongeza pato la serikali kupitia kodi mbalimbali.

"Mkakati huu utajumuisha kuimarisha mtandao wa barabara kuu ili kuunganisha maeneo yote ya uzalishaji na masoko, kupunguza gharama za usafirishaji na kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa katika maeneo haya ya viwanda zinawafikia wateja kwa haraka na ufanisi mkubwa," alisema Dk. Mwinyi.

> **"Mkakati huu utajumuisha kuimarisha mtandao wa barabara kuu ili kuunganisha maeneo yote ya uzalishaji na masoko, kupunguza gharama za usafirishaji na kuhakikisha bidhaa ...**

Pia aliwahakikishia wawekezaji wote kuwa serikali itaendelea kutoa msaada unaohitajika ili kuharakisha uwekezaji unaokusudiwa kufikia malengo yake.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema watahakikisha wanaweka sera madhubuti katika kuzalisha bidhaa ambazo zitatoa nguvu za ushindani kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.


Alisema walikuwa na nyakati ngumu ya kuwaeleza wananchi umuhimu wa mradi huo, kwamba yamejumuisha maeneo matatu ikiwamo kiwanda cha utengenezaji wa dawa za binadamu na chanjo, kiwanda cha kuunganisha vyombo vya moto na maabara ya taasisi ya viwango.

Alisema ahadi ya wizara hiyo ni kuendeleza ndoto ya sera za viwanda na wizara imekamilisha ajenda ya mageuzi ambayo inaainisha maeneo yote ya kibiashara na viwanda ambayo yanakwamisha maendeleo ya viwanda kufanyiwa kazi.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Fatma Khamis, alisema eneo hilo litafungua fursa nyingi za kiuchumi na kijamii, lina ukubwa wa ekari 173.

Alisema kabla ya kuanza mradi, Wizara ililipa fidia ya mazao na majengo kwa wananchi 41 wa eneo hilo na Sh. milioni 590.7 zilitumika kulipa fidia.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud, alisema wamepokea mradi huo kuazishwa katika mkoa huo ambao utaondoa tatizo la ajira.



Balozi wa Heshima wa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Ali Mohammedraza Dewji (katikati), akiwa pamoja na Ofisa Mkuu wa Ustawi wa Jamii wa mkoa huo, Nyamala Elisha (kulia) na Ofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Temeke, Lilian Mafole, wakati wa mkutano wa wadau wa sekta ya ustawi wa jamii, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi akoshwa utendaji kazi Waziri wa Biashara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, amesema ameridhishwa na utendaji kazi wa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, ambaye anatoka Chama cha ACT-Wazalendo.

Alitoa pongezi hizo juzi baada ya hafla ya utiaji saini wa hati za makabidhiano ya eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha dawa za binadamu na chanjo pamoja na kiwanda cha kuunganisha magari katika Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema utendaji wa waziri huyo ni mzuri na kuwataka viongozi wengine wa nafasi za uteuzi wasikubali kuondoka katika nafasi waliopewa bila ya kuacha alama katika kipindi ulichokuwapo.

"Nataka niseme leo hadharani kwamba naukubali sana utendaji wenu Wizara ya Biashara ikiongozwa na Waziri Omar Said Shabani, mnafanya kazi nzuri na mara zote nikiteua watu huwa na kauli moja nawaambia msikubali kuondoka katika nafasi uliopewa bila ya kuacha alama kwa kipindi ambacho ulikuwapo," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema Wizara ya Biashara imeacha alama katika utendaji wao wa kazi anazozifanya waziri wa wizara hiyo ni kama anatoka CCM.

Alisema serikali imepewa kazi kupitia Ilani ya CCM ni kuyapima na kuyaweka tayati maeneo ya viwanda ambapo kwa sasa wamevuka malengo ya ilani hiyo. Dk. Mwinyi alisema matarajio yake hadi ifikapo kipindi cha pili cha uongozi wake baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 atakuwa ameacha alama katika sekta ya viwanda.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**IRENE AVITI TIRA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya kidato cha nne na cha sita vyenye index namba **S0264-0054 na S0264-0535** vilivyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BARBRO JOHANSSON MODEL GIRL'S SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017 na 2020 na cheti cha chuo chenye usajili namba 2632009/t.20 kilichotolewa na **MZUMBE UNIVERSITY** mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/151462/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAIDI AWADHI MPERELLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0620/0231/2013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TEGETA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/162866/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**SALOME HAMIS MASANYIWA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 121362,** iliyotolewa makao makuu PCO, DAR ES SALAAM mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI **CONTROL NUMBER: 9910841993197**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ABDULKARIM FARID NASSOR** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye usajili namba **MC 215 DEH.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/106769/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMIR MUHAMMED ATIBU** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili namba **MC 471 DQX.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN59109/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya ..KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la madai Na 194/2024**

**Jina la mdai............MAKTAUWO CONSULTANTS CO. LTD**

**Jina la Mdaiwa ..................................JOSELINE MAKUNDI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JOSELINE MAKUNDI**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 14 mwezi 8 mwaka 2024 saa 3:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 1 mwezi 8 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IGUNGA**

**MAOMBI YA ARDHI NA. 16 YA MWAKA 2023**

**MWANUKUZI KASEKO ........................................ MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **LINDA CHIKULI**
2. **KIKULI KASEKO**
3. **NGOLO KASEKO**
4. **MASHAKA KASEKO**
5. **MUSOMA KASEKO......................................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

Wajibu maombi **NGOLO KASEKO na MASHAKA KASEKO** popote mlipo mnafahamishwa kwamba **BW. MWANUKUZI KASEKO** amefungua maombi ya Ardhi Na. 16/2023 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lililopo Nzega. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 15/08/2024 saa 2:30 asubuhi. Hivyo mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W) – Nzega.
Mfahamu kwamba msipohudhuria maombi husika yatasikilizwa bila ya nyinyi kuwepo/kutoa utetezi wenu na kutolewa hukumu Imetolewa na kutiwa saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 19/072024.

V. A.LING'WENTU
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
NZEGA

---

**FORM MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya.....TANGA**

**Kituo cha......PONGWE............... Mkoa...................TANGA**

**Usimamizi wa wa Mirathi Na........14......./2024...............**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU.......................MASHAKA ALBERTO JACKOBO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA .................................MGINA MASHAKA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tar .....02 ... mwezi....09... mwaka.....2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**ZINGATIA;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo Tarehe.....06..... mwezi...8... mwaka....2024

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATES COURT OF ARUSHA AT ARUSHA**

**SMALL CLAIM NO 16397 OF 2024**

**TATA AFRICA HOLDINGS (TANZANIA ) LIMITED...CLAIMANT**

**VERSUS**

**SILKY TRACTORS AND EQUIPMENTS PARTS (T) LIMITED...............................RESPONDENT**

**TO:**
**SILKY TRACTORS AND EQUIPMENTS PARTS (T) LIMITED**

**NOTICE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing in the Resident Magistrates court of Arusha at Arusha on the 15th day of August, 2024 at 09:00 AM in the forenoon, you may appear in person or your advocate

**TAKE FURTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day and time for hearing, the court may proceed in absence.

**GIVEN under my HAND** and seal of the court this 1st day of AUGUST, 2024

Senior Resident Magistrate
Arusha

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAYURI YA JIJI LA DODODMA**

**OFISI YA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA IMEPOKEA MAOMBI YA KUMILIKISHWA KIWANJA NAMBA 15 KITALU "B" ENEO LA MKAMALA KUTOKA KWA NDUGU EDWIN M. KUSUNDWA WA S.L.P 1 DODODMA.**

**HATA HIVYO, KABLA YA KUENDELEA KWA HATUA ZAIDI, MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA ANAUTANGAZIA UMMA KUWA, KAMA KUNA MWANANCHI/TAASISI/KAMPUNI AU KIKUNDI ANA/KINA MASLAHI/MAONI YOYOTE JUU YA KIWANJA TAJWA AWASILISHE KWA MAANDISHI MASLAHI/MAONI HAYO KWA MKURUGENZI WA JIJI NDANI YA SIKU (30) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.**

**BAADA YA MUDA HUO KUPITA BILA TAARIFA YOYOTE, OFISI ITAENDELEA NA HATUA ZAIDI**

Adinani L. Omari
Afisa Ardhi Mteule
Kny: MKURUGENZI WA JIJI - DODOMA.

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi amtuhumu Kabila kusaidia waasi M23

**KINSHASA,** DRC

**Nchi hizo mbili majirani wiki iliyopita zilikubaliana kusitisha mapigano kuanzia Jumapili, baada ya kufanyika kwa mazungumzo nchini Angola.**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, amemshushia tuhuma kiongozi wa zamani wa taifa hilo, Joseph Kabila, kuwa anaunga mkono muungano wa makundi ya waasi wanaotaka kupindua serikali yake.

Kiongozi huyo alitoa tuhuma hizo wakati wa mahojiano na kituo binafsi cha redio juzi.

Rais Tshisekedi, alinukuliwa akisema wakati wa mahojiano hayo kuwa Kabila alisusia uchaguzi na anapanga kuanzisha uasi kwa kuunga mkono muungano huo wa makundi ya waasi unaojulikana kama AFC.

Muungano huo unadaiwa kuwa vuguvugu la kisiasa na kijeshi ulioanzishwa mwezi Desemba kwa lengo la kuyaunganisha makundi yote yenye silaha, vyama vya siasa na asasi za kiraia yanayoipinga serikali ya DRC.

Hata hivyo, Kabila amekanusha madai hayo akieleza Rais Tshisekedi hafahamu historia ya mapigano mashariki mwa nchi hiyo, na sasa ametunga uongo ili kujilinda.

Shutuma hizo za Tshisekedi zinafuatia tangazo la Marekani la kuuwekea vikwazo muungano huo lililotolewa mwezi uliopita.

Marekani inaushutumu muungano huo kwa kujaribu kuipindua serikali ya DRC na kuchochea mzozo mashariki mwa nchi nchi hiyo.

Katika taarifa yake ilisema kuwa mwanachama mkuu katika muungano huo kundi la waasi la M23, tayari liko kwenye vikwazo.

Rais Tshisekedi, pamoja na wataalamu wa Marekani na Umoja wa Mataifa, waliishutumu nchi ya Rwanda kwa kusaidia kijeshi kundi la M23.

Rwanda inakanusha madai hayo, lakini mwezi Februari ilikiri kwamba ina vikosi vya kijeshi na mifumo ya makombora mashariki mwa DRC ili kulinda usalama wake, ikitaja ongezeko la vikosi kijeshi kuwa karibu na mpaka.

Nchi hizo mbili majirani wiki iliyopita zilikubaliana kusitisha mapigano kuanzia Jumapili, baada ya kufanyika kwa mazungumzo nchini Angola.

Eneo la Mashariki mwa Kongo limekuwa likikabiliwa na ghasia huku zaidi ya vikundi 120 vikipigania udhibiti wa ardhi na rasilimali muhimu za madini. **DW**



Polisi wa kutuliza ghasia walikabiliana na waandamanaji katika eneo la Bristol, kusini mwa Uingereza, kwenye maandamano yanayoendelea nchini humo. **PICHA: AFP**

# Polisi 6,000 kudhibiti ghasia

**LONDON,** Uingereza

POLISI 6,000 wa kupambana na ghasia wameripotiwa kuwa tayari kusambazwa nchini Uingereza kwa ajili ya kukabiliana na machafuko yanayoendelea katika maeneo mbalimbali.

Ghasia hizo zilianza wiki iliyopita baada ya watoto wawili kuuawa na kijana mwenye asili ya Afrika.

Makundi kutoka mrengo wa kulia yalipanga kushiriki maandamano hayo katika maeneo zaidi ya 30, yakilenga ofisi za mawakili wanaowatetea wahamiaji na majengo yanayotoa hifadhi kwa waomba hifadhi.

Kulingana na taarifa ya serikali, polisi hao kutoka katika vitengo maalumu wamethibitishwa kuwa wako tayari kukabiliana na waandamanaji.

Ghasia hizo ndio mbaya zaidi kuwahi kutokea nchini Uingereza katika kipindi cha mwongo mmoja.

Vurugu hizo zilianza baada ya wasichana watatu wenye umri kati ya miaka tisa, saba na sita kuuawa na wengine zaidi ya watano walijeruhiwa baada ya kushambuliwa na mtu aliyekuwa amejihami kwa kisu.

Hata hivyo, taarifa za kupotosha zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii kwamba mshambuliaji huyo alikuwa mwisilamu ambaye ni mhamiaji.

Baada ya muda mshukiwa wa shambulio hilo alibainika kuwa ni Axel Rudakubana mtoto wa miaka 17 mzaliwa wa Wales ambaye wazazi wake wanatokea nchini Rwanda.

Waziri Mkuu, Keir Stamer, alionya kuwa yeyote atakayehusika na machafuko hayo atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na wale wanaochochea vurugu kupitia mitandao. **RFI**

# Al-Sinwar kiongozi mpya Hamas

**GAZA,** Palestina

KUNDI la Hamas linalotawala Ukanda wa Gaza limemteua Yahya al-Sinwar kuwa kiongozi mkuu wa kisiasa na kuchukua nafasi ya marehemu Ismail Haniyeh ambaye aliuawa wakati akiwa nchini Iran.

Kuteuliwa kwa kiongozi huyo kunaambatana na hali ya wasiwasi katika ukanda wa Mashariki ya Kati ikijiandaa na uwezekano wa mashambulizi ya Iran na washirika dhidi ya Israel.

Sinwar, anashutumiwa na Israel kuwa kinara wa mashambulizi ya Oktoba 7 yaliyofanyika kusini mwa Israel, yaliowauwa takribani watu 1,200, na wengine wapatao 250 wamechukuliwa mateka.


Hata hivyo, kwa karibu miezi 10 ya mashambulizi ndani ya Ukanda wa Gaza, Al-Sinwar amevikwepa vikosi vya Israel vinavyomsaka kwa udi na uvumba.

Haniyeh aliyekuwa na makao yake nchini Qatar, aliuawa takribani wiki moja iliyopita katika shambulio la kulenga lililodaiwa kufanywa na Israel, wakati akiwa ziarani mjini Tehran kuhudhuria uapishwaji wa Rais mpya wa Iran.

Kuchaguliwa kwa Al Sinwar mwenye urafiki wa karibu na Iran na aliyetoa mchango mkubwa katika kuijenga Hamas, kunatazamwa kama ishara ya kuwa kundi hilo limejiandaa kuendeleza mapambano.

"Tunazingatia kwamba kuchaguliwa kwa Sinwar kunamaanisha uzinduzi mpya kwa ajili ya hatua mpya ambayo Sinwar atawasilisha, Mungu akipenda, kutakuwa na mengi zaidi baada ya hatua hiyo. Na tutawasilisha, kujitolea zaidi kwa ajili ya kuikomboa Palestina, Mungu akipenda," alisema Rabih Radwan, mwakilishi wa Hamas mjini Saida, nchini Lebanon

Tangazo la kuchaguliwa kwa Al-Sinwar limeibua hofu kwamba huenda likaikasirisha Israel na kuchochea vita zaidi, wakati viongozi wa juu wa Marekani wakiendelea na juhudi za kidiplomasia kuishinikiza nchi hiyo na Iran kuepusha mzozo mpana zaidi. **DW**



# Kiongozi mpya aomba utulivu Bangladesh

**DHAKAR,** Bangladesh

KIONGOZI wa muda nchini Bangladesh, Muhammad Yunus, ametoa wito kwa raia kuwa watulivu na kuwa tayari kuijenga upya nchi yao.

Mwanauchumi huyo aliteuliwa kuongoza serikali ya mpito baada ya Waziri Mkuu, Sheikh Hasina kukimbia nchi hiyo kufuatia maandamano ya wananchi waliopinga ukosefu wa kazi na utawala mbaya.

Kiongozi huyo ambaye kwa sasa yuko Ulaya atarejea nchini humo leo, alitoa wito huo katika jarida la Uingereza la The Economist.

Aliahidi kwamba atafanya kila kitu kuhakikisha uchaguzi huru na wa haki katika miezi michache ijayo. **RFI**

# KOCHA COASTAL, DODOMA JIJI AIBUKIA MTIBWA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mtibwa Sugar imemtangaza kocha wa zamani wa klabu za Coastal Union na Dodoma Jiji, Melis Medo kuwa Kocha Mkuu kwa ajili ya kukinoa kikosi hicho kwenye Ligi ya 'Championship'.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema kuwa, kocha huyo raia wa Marekani, ameingia mkataba wa mwaka mmoja lengo likiwa ni kujaribu kuirudisha timu hiyo Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuteremka mwishoni mwa msimu uliopita.

"Tuna furaha kumtambulisha kocha Medo, ambaye atakuwa kocha wetu mkuu kwa msimu wa 2024/24", ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

**Tayari kocha huyo ameanza kazi akiwa na kikosi hicho ambacho kinajiandaa na michezo ya Ligi ya Championship.**

Kocha huyo ameshawahi kufundisha soka katika vilabu mbalimbali nchini Kenya na Tanzania ambapo amezifundisha vilabu vya Coastal Union na Dodoma Jiji.

Mtibwa Sugar ilishuka daraja baada ya kuburuza mkia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, ikiambulia pointi 21 tu katika michezo 30 iliyocheza, ikishinda michezo mitano, sare sita na kupoteza michezo 19.

Kwa mara ya kwanza ilipanda daraja mwaka 1995 na kufanikiwa kutwaa ubingwa mwaka 1999 na 2000 na imedumu kwenye ligi kwa miaka 29, kabla ya kushuka msimu uliopita.

Wakati huo huo, timu hiyo imewasajili wachezaji wawili wapya, Anuar Jabir ambaye ni straika kutoka Dodoma Jiji na Amani Kyata kutoka Namungo ili kujiimarisha katika azma yao ya kufanya vizuri championship na kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

# *Mbunge wa Ngara awapa somo wanamichezo*

**Na Judith Julius,** Ngara

WANARIADHA na wanamichezo wa Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, wametakiwa kuendelea kufanya mazoezi, kwa kufanya hivyo watazidi kujiimarisha na kuwa na afya njema.

Wito huo umetolewa jana na mbunge wa jimbo hilo, Ndaisaba George Ruhoro wakati akizungumza na wanariadha walioshiriki katika mbio za nusu marathoni zilizopewa jina la 'Ngara Ruhoro Nusu Marathon', zilizofanyika wilayani humo mwishoni mwa wiki.

Washiriki wa mbio hizo ambazo kwa sehemu kubwa zilishirikisha wanariadha wa wilayani humo, walikimbia mbio za kilomita 5, 10, na 21.

Mbio hizo zilianzia Uwanja wa Posta ya zamani na kwenda barabara kuu iendayo nchini Burundi.

"Nipo tayari kushirikiana na washiriki waliofanya vizuri kuendeleza vipaji vyao kwa kuwawezesha kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ili kujinufaisha kiuchumi," alisema Ruhoro.



Aidha, alisema wananchi wa wilaya hiyo waanzishe utaratibu wa kufanya mazoezi kila wakati ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Kwa upande wake, Ofisa Utamaduni wa Wilaya hiyo, Said Salum, alisema mwitikio wa wanariadha kushiriki katika mbio hizo ulikuwa mzuri sana kuliko ulivyokuwa hapo awali kwani mwamko wa wananchi ni mzuri katika kushiriki michezo.




Kamishna wa Shirikisho la soka Duniani (FIFA) na lile la Afrika (CAF), Somoe Ng'itu akiwa anaonesha fomu ya kuwania uwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu wa Wanawake Tanzania (TWFA), katika uchaguzi utakaofanyika Septemba 14, mwaka huu mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BTMZ yafuta mchezo mpya Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BARAZA la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ) limetangaza kuupiga marufuku na kuufungia mchezo wa mbio za magari 'drifting' hadi utakapokamilika mchakato wa kuruhusu mchezo huo.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa jana, Katibu Mtendaji wa BTMZ, Said Marine, alisema Agosti 4, mwaka huu huko Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, lilifanyika shindano la mchezo huo bila ya kupata kibali kutoka BTMZ jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Alisema mchezo huo wa 'kuseresha magari' kwa sasa umesimamishwa mpaka hapo utakapowekewa kanuni na mazingira rafiki ya kusimamiwa na uendeshwaji wake katika mazingira rafiki na yaliyo salama bila kuathiri watu wengine.

Alisema serikali kupitia BTMZ imepiga marufuku mchezo huo ili kutafuta namna bora ambayo itaweza kuweka mazingira mazuri kwa watazamaji na hata maeneo ya kufanyika mchezo huo.

Aidha, alisema BTMZ inafahamu umuhimu wa mchezo huo na namna unavyoweza kuleta fursa nyingi kwa vijana kujiajiri kutoka na wachezaji wa mchezo huo kulipwa fedha nyingi.

"Michezo yote inafaida kubwa kwenye nyanja mbalimbali katika nchi, lakini lazima kuwe na mazingira rafiki bila kuleta athari kwa wachezaji na hata watazamaji," alisema Marine.

Alisema serikali inaandaa kanuni za mchezo huo kwa kushirikiana na wadau, ambapo kwa kuanzia wataanzisha chama cha mchezo huo.

Katika hatua nyingine, Baraza hilo limewataka waandaaji wa mashindano ya 'Ndondo' hapa nchini kuhakikisha wanaratibu vizuri na kusimamia suala la usalama viwanjani kwani kumeibuka vikundi vinavyotoa burudani katika michezo mbalimbali kwa kuimba nyimbo zinazohamasisha matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kushindwa kufanya hivyo baraza litachukua hatua kali za kisheria kwa waandaaji au waratibu wa mashindano hayo yanayoendelea katika kipindi hiki.

**Michezo yote inafaida kubwa kwenye nyanja mbalimbali katika nchi, lakini lazima kuwe na mazingira rafiki bila kuleta athari kwa wachezaji na hata watazamaji.**

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL imebakia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Napoli na timu ya taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, 25, licha ya kutakiwa na PSG. ***(Gianluca di Marzio via X)***

### BRIGHTON YAMSAKA HUMMELS

KLABU ya Brighton imefanya mawasiliano na mchezaji huru, beki wa zamani wa Bayern Munich na Borussia Dortmund, Mats Hummels, 35, ambaye alishinda Kombe la Dunia akiwa na Ujerumani mwaka 2014, ingawa wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa West Ham. ***(Sky Sports)***

### UNITED KUSAMJILI BERGE

MPANGO wa Manchester United wa kusaka kiungo unaweza kuwafanya watoe ofa ya kumnunua mchezaji wa kimataifa wa Norway na Burnley, Sander Berge, 26, baada ya klabu hiyo ya Old Trafford kukataa kumsajili mchezaji wa PSG raia wa Uruguay, Manuel Ugarte, 23. ***(Athletic)***

### OLMO, BARCA MAMBO SAFI

BARCELONA imefikia makubaliano ya mazungumzo juu ya ada ya pauni milioni 47.3 pamoja na nyongeza ya pauni milioni sita na RB Leipzig kwa kiungo mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo, 26. ***(Fabrizio Romano on X)***

### SOLANKE AIVUTIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mshambuliaji wa Bournemouth, Dominic Solanke, lakini uhamisho wa Muingereza huyo unaweza kutegemea mustakabali wa mshambuliaji wa Brazil Richarlison kwenye klabu hiyo. ***(Standard)***

### RICHARLISON NA SAUDIA

KLABU ya Tottenham Hotspurs inajiandaa kupokea ofa kubwa kwa ajili ya mshambuliaji wake Richarlison kutoka Ligi Kuu ya Saudia. ***(Football Insider)***

### BAYERN, TAH MAMBO BADO

KLABU ya Bayern Munich bado hawajafanikiwa katika mazungumzo yao na Bayer Leverkusen kuhusu kumnunua beki wa Ujerumani, Jonathan Tah, 28. ***(Sky Germany)***

### O'SHEA AWANIWA BRENTFORD

KLABU ya Brentford imewasilisha ombi la pauni milioni 7 kumnunua beki wa Burnley kutoka Jamhuri ya Ireland, Dara O'Shea mwenye umri wa miaka 25. ***(HITC).***

### EWIJK AWA LULU UHOLANZI

KLABU ya Ajax, Feyenoord na PSV zote zina nia ya kumsajili beki wa kulia wa Coventry City Mholanzi, Milan van Ewijk, mwenye miaka 23. ***(ESPN)***

### MILANGO IKO WAZI KWA INGS

KLABU ya West Ham iko tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa England, Danny Ings mwenye umri wa miaka 32. ***(Football Insider)***

## DONDOO KUTOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN MUNICH KUMPIGA BEI DAVIES

**● ● ● Beki huyo anawindwa zaidi na mabingwa wa Ulaya, Real Madrid huku Wajerumani...**

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich bado inaweza kumuuza mchezaji anayesakwa na Real Madrid, Alphonso Davies msimu huu wa majira ya joto baada ya kuamua kutompa beki huyo wa kushoto mkataba mpya.

**Kwa hali ilivyo, Davies yuko mbioni kuwa mchezaji huru msimu ujao mkataba wake wa sasa utakapomalizika.**

Mazungumzo katika miezi ya hivi karibuni bado hayajaleta makubaliano juu ya mkataba mpya, huku kambi ya mchezaji huyo na Bayern zikiwa ziko mbali sana katika nafasi zao za mazungumzo.

Akiwa na matumaini ya kuonyesha hadhi yake kama mmoja wa mabeki wa pembeni bora zaidi duniani, Davies ameripotiwa kuomba kiasi cha euro mil 20 kwa msimu, ikilinganishwa na ofa ya Bayern ya euro mil 13.

Masharti yake ya sasa yalitiwa saini mwaka 2020, kabla hajashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lakini rais wa heshima wa Bayern, Uli Hoeness alionya mwezi uliopita kwamba klabu hiyo haitampatia mchezaji huyo 'fedha zaidi'.

Msimamo huo unaonekana kuwa mstari thabiti kwenye mchanga ambao utachagiza hatua inayofuata ya sakata hili. Mwanahabari Maximilian Koch emesema Bayern wameamua kutotoa mkataba mpya na kumwacha Davies kuamua kama anataka kuukubali au la.

Lakini badala ya kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kumaliza mkataba wake na kuondoka bila ada ya uhamisho kama ilivyodaiwa awali, kuuzwa katika majira haya ya joto bado inawezekana.

Real Madrid ndio klabu inayohusishwa zaidi na Davies.

Lakini mabingwa hao wa Ulaya tayari wameingia sokoni na kumnasa Kylian Mbappe kwa mshahara na kusaini bonasi badala ya ada ya uhamisho pamoja na kindawa Brazail, Endrick.

# ONANA AAHIDI FURAHA KWA MASHABIKI




**MANCHESTER,** England

MLINDA mlango wa Manchester United, Andre Onana, amebainisha kuwa ana nia ya kuimarika zaidi huku klabu hiyo ikilenga kampeni bora katika msimu wa 2024/25.

Onana alivumilia msimu wa kwanza mgumu baada ya uhamisho wa pauni milioni 47.2 kutoka Inter Milan na kufanya makosa kadhaa katika mazingira mapya.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon hajaahirisha kuvuka mipaka katika hali ya hatari na amewahakikishia mashabiki kutarajia makubwa zaidi.

"Huyo ni mimi, na nadhani ndivyo utakavyoona msimu huu kwa sababu nitaimarika zaidi. Ninaweza kukuambia mapema tayari," alisema Onana akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Jumamosi wa Ngao ya Jamii.

"Jiandae kwa sababu utakuwa msimu huu, niamini! Nitafurahia zaidi msimu huu utakapoanza.

"Kwangu mimi, ni muhimu kutambua mambo ya aina hiyo na kufanya uamuzi bora kwa timu. Nitachukua jukumu kubwa na nadhani mgongo wangu ni mkubwa kubeba yote. Nadhani utakuwa msimu mzuri sana."

## Olmo rasmi mali ya Barca



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA walifikia makubaliano kimsingi na Leipzig Jumanne kuhusu uhamisho wa kiungo Dani Olmo kwenda kwa wababe hao wa LaLiga, kwa mujibu wa ESPN.

Utiaji saini unasubiri makubaliano ya mwisho na uchunguzi wa afya leo Alhamisi.

Olmo, tayari yuko Barcelona na wakala wake na anapaswa kuungana na wachezaji wenzake wapya wa Barca mazoezini Ijumaa.

Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, Deco alikutana na wawakilishi wa Leipzig Jumanne asubuhi kwa matumaini ya kukamilisha usajili huo, kwa euro milioni 60.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania amekuwa shabaha kuu ya Barca katika dirisha hili la usajili baada ya miamba hao wa Katalunya kushindwa kumsajili fowadi wa Athletic Club, Nico Williams.

"Tuko tayari kulizungumzia," Schäfer alisema katika mkutano na waandishi wa habari Jumanne alipoulizwa kuhusu nia ya Barca kwa Olmo.

"Lakini Dani ana thamani fulani. Dani ni mchezaji wa kipekee."

Barca tayari wamekubali makubaliano ya kibinafsi na Olmo, ambaye ana nia ya kurejea katika klabu aliyoanzia soka.

Olmo alifunga mabao matatu kwenye michuano ya 'Euro 2024' na kumaliza kama mshindi wa pamoja wa Kiatu cha Dhahabu na kusaidia Hispania kushinda ubingwa wa michuano hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake na Leipzig unamalizika Juni 2027, amefunga mabao 29 katika misimu yake minne katika klabu hiyo.

## Gundogan hana mpango na Fenerbahce

**BARCELONA,** Hispania

ILKAY Gundogan hatarajiwi kuzingatia ofa za uhamisho msimu huu, licha ya Barcelona kuwa tayari kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 iwapo ofa itatokea.

Gundogan alijiunga na wababe hao wa Katalunya kwa uhamisho wa bila malipo msimu uliopita baada ya kuwa nahodha wa Manchester City hadi kutwaa mataji matatu ya Ligi Kuu, Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alichangia mabao 19 na asisti katika mechi 51 katika mashindano yote na alikuwa kiungo anayetegemewa zaidi kikosini.

Lakini mapungufu ya kifedha ya Barcelona yamesababisha mabadiliko makubwa ya wachezaji katika miaka ya hivi karibuni na Gundogan amekuwa akihusishwa kuhama.

Mundo Deportivo limeandika kwamba Gundogan, kupitia wakala wake na mjomba wake, Ilhan, ameifahamisha Barcelona kwamba hana nia ya kufikiria ofa kutoka kwingineko.

Hiyo ni kwa sababu ana furaha katika jiji hilo na ana nia ya kuacha alama yake kwenye klabu kwa kupata kitu "kikubwa".

Msimamo wa Barcelona ulikuwa kuzingatia ofa zilizoletwa kwao na kambi ya Gundogan ikiwa itachukuliwa kuwa inafaa na pande zote.

Gundogan anaripotiwa kutakiwa Uturuki huku Jose Mourinho akiwa mstari wa mbele kumtaka kwenye timu yake ya Fenerbahce kutokana na jeraha alilopata kiungo wa zamani wa Manchester United, Fred kwenye klabu hiyo.

Miamba hao wa Istanbul hawajakosa matarajio katika soko la uhamisho huku wakijaribu kutetea tena utawala wa ndani baada ya msimu uliopita kuadhimisha miaka kumi kamili bila taji la Super Ligi.



HABARI MICHEZO

# KLABU 24 BADO HAZIJAFANYA USAJILI, ZIPO TATU ZA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwangwo**

ZIKIWA zimebaki siku saba tu kabla ya kufungwa kwa dirisha kubwa la usajili kwa madaraja mbalimbali nchini, jumla ya timu 24 bado hazijafanya usajili, zikiwamo tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, (TFF), imesema kuwa hadi jana klabu hizo bado zilikuwa hazijaingiza majina ya wachezaji wake ambao itawatumia kwa msimu ujao wa mashindano.**

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, imezikumbusha klabu zote kuwa mwisho wa usajili ni Agosti 15, saa 5:59 usiku na hakutakuwa na muda wa ziada.

Imezitaja timu ambazo mpaka sasa bado hazijafanya usajili kwa timu za Ligi Kuu kuwa ni Tabora United, Fountain Gate na Dodoma Jiji.

Hata hivyo, TFF, imesema Tabora United na Fountain Gate zenyewe zimefungiwa kufanya usajili mpaka zitakapowalipa wachezaji wanaowadai.

Kwa upande wa timu za Ligi ya 'Championship' ambazo hazijakamilisha usajili wa wachezaji wake kwenye mfumo ni Biashara United, Mbeya Kwanza, TMA Stars, African Sports, Mtibwa Sugar, Gaita Gold, Stand United na Songea United. Biashara United ina adhabu ya kufungiwa kusajili, hivyo nayo haiwezi kufanya hivyo mpaka itakapowalipa wachezaji wanaoidai timu hiyo.

Klabu ambayo hazijafanya usajili mpaka sasa Ligi Daraja la Pili, maarufu kama 'First League' ni Tanesco, Nyumbu, Magnet, Tunduru Korosho, Dar City, African Lyon, Gunners FC, Hausing FC, Moro Kids, Pan African na Ruvu Shooting.

Zipo pia timu mbili za Ligi Kuu Wanawake ambazo hazijafanya usajili ambazo ni Ceasiaa Queens na Gets Program.



Mchezaji wa Soka wa Timu ya Vijana ya Jakaya Kikwete, Sunday Haji (kushoto), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Streek Kids, Kassim Said (kulia), wakati wa mechi ya kirafiki katika uwanja wa Kidongo Chekundu jijini Dar es Salaam jana. Timu ya Kituo cha Jakaya Kikwete ilishinda bao 1-0. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Simba, Yanga hapatoshi leo

INATOKA UKURASA 24

mi ladha ya mechi za dabi kati ya timu hizo zenye utani na upinzani wa jadi tangu mwaka 1936.

"Nafikiri Simba Day imetupa mwanga na mwelekeo wa kule tunakoelekea, tumemaliza wiki zetu za maandalizi ya msimu, tunaikabili Yanga ambao ni Mabingwa wa Tanzania Bara, mchezo utatupa ladha ya soka la hapa Tanzania, utatupa na kutuonyesha nini tunatakiwa tufanye kwenye ligi, tunajua ni timu ambayo iko pamoja kwa misimu mitatu na sisi tuna asilimia kubwa ya kikosi kipya, tuna wachezaji wazuri na wenye vipaji hivyo tunataka kushinda mechi hii," alisema kocha huyo.

"Malengo yangu ni kushinda mchezo kwani nina wachezaji wazuri ambao ninaamini wataonyesha ushindani katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Fadlu.

Kwa upande wa Gamondi alisema anajua Simba watakuja kivingine tofauti na msimu uliopita, lakini hajali, atakachofanya ni kuwaambia vijana wake wacheze soka kwa dakika zote 90 ili kupata ushindi.

## WACHEZAJI 147 KUCHUANA 'POOL TABLE' MOROGORO

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI 147 wanatarajia kuchuana katika mashindano ya Ubingwa wa Taifa ya mchezo wa 'pool table' yanayoanza leo mpaka Agosti 10 kwenye Ukumbi wa Samaki Samaki mjini Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Mchezo huo Tanzania, (TAPA) Abdallah Omar Abdallah, alisema kati ya wachezaji hao, wanaume ni 128 huku wanawake wakiwa 16 na wenye mahitaji maalum wakiwa watatu.

Abdallah, alisema maandalizi ya mashindano hayo yamekamilika kwa asilimia 100 huku matarajio yao kuona wanapata kile walichokusudia.

"Kesho (Leo) tunaanza mashindano yetu ambayo lengo ni kutafuta viwango vya wachezaji pamoja na kuchagua timu ya Taifa ambayo itashiriki Mashindano ya Dunia yatakayofanyika Oktoba Mwaka huu nchini Uingereza," alisema Abdallah.

Alisema kuwa kutakuwa na zawadi kwa washindi mbalimbali kuanzia ngazi ya klabu na mshindi mmoja mmoja.

## Ndumbaro awakalia 'kooni' viongozi TPBRC

INATOKA UKURASA 24

ngumi na kusababisha vijana wengi kukosa ajira.

"Ukikosa uthibitisho kwenye matumizi huo ni wizi, lazima ulete nyaraka za uthibitisho zinazoonesha jinsi fedha hizo zilivyotumika kwani hizo ni fedha nyingi ambazo mabondia wametumia jasho lao," alisema Ndumbalo.

Aidha, aliipongeza kamati hiyo ya uchunguzi kutokana na kufanya kazi yao kwa weledi na kubaini hoja ambazo zina mashiko makubwa.

Katika hatua nyingine alimtaka msajili wa vyama vya michezo nchini, Evodi Kyando, aipitie ripoti hiyo ili aweze kuchukua hatua stahiki dhidi ya viongozi hao.

"Msajili uchukue hatua kali, zile za jinai zipelekwe kwenye vyombo vya husika, viongozi wahusika waendelee kusimamishwa mpaka hapo msajili atakaposema wana hatia au vinginevyo bila upendeleo wala kuonea mtu yeyote," alisema Ndumbaro.

Hata hivyo, aliongezea siku 90 nyingine kamati hiyo kutokana na kuridhishwa na kazi iliyofanya pamoja na kuwaongeza viongozi wengine ambao wataungana na kamati hiyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi Christopher Kamugisha alibainisha hoja 13 walizozibaini katika kipindi chao cha siku 90 wakati alipokuwa akikabidhi ripoti yao.

"Kamati ilibainisha mambo 13 na miongoni mwa mambo vitu tuliyoyabaini ni kamisheni kuongozwa na watu wawili. Vilevile, tulibaini walimsainisha mkataba bondia ambaye alikuwa si Mtanzania pamoja na kutoshirikisha vyama husika na kutokutoa leseni kwa wakati," alisema Mugisha.

# Michezo

Alhamisi Agosti 8, 2024

Nipashe




Onana aahidi furaha kwa mashabiki UKURASA 22

# Simba, Yanga hapatoshi leo, kila kocha asifu nyota wake

## Ni katika mchezo wa Ngao ya Jamii, huko Zanzibar Coastal...



**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akisema hajui Simba itaingia na mfumo gani kutokana na kuwa na wachezaji wengi wapya pamoja na benchi la ufundi, mwenzake wa Simba, Fadlu David, amesema anaamini vijana wake wana uwezo mkubwa wa kupambana ili kushinda mechi.

**Wakongwe wa soka la Tanzania, Simba na Yanga leo watashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii, ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2024/25, mchezo huo utaanza saa 1:00 usiku.**

Mchezo huo utatanguliwa na ule wa nusu fainali ya kwanza utakaochezwa saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa New Amaan Stadium, Zanzibar kwa kuzikutanisha Azam FC na Coastal Union.

Mshindi katika kila mchezo atasonga mbele kucheza fainali, Agosti 11 kwenye uwanja huo kuwania Ngao ya Jamii.

Mchezo wa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa utakumbushia pambano la fainali ya Ngao ya Jamii lililochezwa mwaka jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Simba ikitwaa taji hilo kwa kushinda mabao 3-1, yaliyopatikana kwa mikwaju ya penalti, baada ya dakika 90 za suluhu.

Mchezo wa leo unasubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi si Tanzania tu au Ukanda wa CECAFA, bali Afrika nzima kutokana na mvuto wa soka la Tanzania.

Itashuhudiwa kwa mara ya kwanza, Yanga ikichezesha wachezaji wapya waliosajiliwa msimu huu, kama Clatous Chama aliyetokea Simba, ambaye ataingia kwenye rekodi ya kucheza dabi akiwa na klabu zote mbili, Prince Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC, Duke Abuya aliyetokea Singida Big Stars, na Aziz Andambwile wa Singida Fountain Gate.

Simba itaingia uwanjani ikiwa na idadi kubwa ya wachezaji wapya waliosajiliwa msimu huu kiasi kwamba hata mashabiki wao hawawezi hata kutabiri kikosi cha kwanza kitakuwaje.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wachezaji ambao wameonekana kuwa kivutio kwenye mchezo wa kilele cha Tamasha la Simba Day, kama kipa, Moussa Kamara, Joshua Mutale, Jean Charles Ahoua, Debora Fernandes Mavambo, Augustine Okejepha, Awesu Awesu na Kelvin Kijili.

Kocha Mkuu wa Simba, raia wa Afrika Kusini, Fadlu, leo ataonja ras-

INAENDELEA UKURASA 23



# Ndumbaro awakalia 'kooni' viongozi TPBRC

**Na Shufaa Lyimo**

WAZIRI wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, ametoa siku saba kwa viongozi wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa (TPBRC) kuwasilisha nakala 170 za mikataba ofisini kwake.

Maagizo hayo ya Ndumbaro yamekuja baada ya kamati aliyoiunda miezi mitatu iliyopita kuwasilisha kile walichokibaini kwenye uongozi wa kamisheni hiyo ambao ulisimamishwa na serikali.

Katika taarifa yake, kamati hiyo imeainisha hoja 13 ambazo miongoni mwake zipo za matumizi ya fedha shilingi milioni 183.3 ambazo hazina maelezo, lakini pia kupotea kwa nakala hizo 170 za mikataba mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salam jana, Ndumbaro alisema endapo viongozi hao hawatafuata maagizo hayo, watafikishwa kwenye vyombo vya sheria kwani wameliibia taifa, wadau wa ngumi, Mmlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na mabondia.

"Natoa agizo kwa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kupitia kwa Katibu Mtendaji wake, Neema Msitha, nataka nakala hizo zinifikie haraka, zisipofika wale wote waliohusika tutawafikisha kwenye vyombo vya dola," alisema Ndumbaro.

Aidha, alisema suala hilo hawatalifumbia macho kwani linachangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma mchezo wa

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002